SportPesa
TZS. 761,374,640
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Butiku** asema Katiba jambo la muhimu

UKURASA 3




**Perisic njiapanda Inter Milan**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumatano Desemba 8, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580788

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Shahidi adai kumkamata Sabaya akiwa na bastola

• **Pia** alikuwa na magazine mbili, risasi 21 na zaidi ya simu 10... *Endelea ukurasa 2*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhi cheti cha pongezi cha ushindi wa mlipakodi bora kilichotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, wakati wa ufunguzi wa kongamano la wawekezaji kiuchumi kuadhimisha Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### MAREKANI YATOA MABILIONI MRADI 'WAACHE WASOME'

SERIKALI ya Marekani, kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), imesherehekea miaka mitano ya mradi wa 'Waache Wasome' wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 14.75 (sawa na...

## 'Wagonjwa msikubali kuuziwa damu ni bure'

UKURASA 3




Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wakishirikiana na vikosi vingine jana kuondoa mabaki katika ghorofa lililoanguka juzi Goba, mkoani Dar es Salaam. Watu wanne walikufa na wengine kujeruhiwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wanaume walalamikia ukatili

UK.2

MICHEZO SIMBA, YANGA 'LITAKUFA JITU' UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

## Wanaume walalamikia ukatili, wake zao kuwanyima unyumba

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

BAADHI ya wanaume mkoani Shinyanga, wamelalamika kufanyiwa ukatili wa kijinsia na wake zao ikiwamo kunyimwa unyumba.

Walibainisha hayo jana wakati dawati la jinsia la Jeshi la Polisi wilayani Shinyanga, lilipokuwa likitoa elimu ya ukatili wa kijinsia katika stendi ya mabasi wilayani hapo.

Mmoja wa wanaume hao, Peter Makalanga, alisema wanawake wamekuwa wakiwafanyia ukatili mkubwa waume zao, kwa kuwanyima unyumba hata ndani ya wiki mbili kwa madai ya kuchoka na kazi.

"Tunashukuru kwa elimu hii ya ukatili wa kijinsia kutuletea hapa stendi, lakini wanaume tunanyanyasika sana siku hizi. Wake zetu wanatunyima unyumba, lakini akijua unachepuka ndipo mgogoro unapoanzia na kufikia hatua ya kupigana," alisema Makalanga.

"Waambieni na wake zetu wasitufanyie ukatili lakini wao ukiwagusa tu tayari wanakimbilia polisi kushtaki. Hiyo si sawa lakini ukiangalia chanzo cha yote hayo ni yeye mweyewe kuninyima unyumba," aliongeza.

Pia alisema na migogoro inapotokea ndani ya familia, ndiyo chanzo cha kuachana na kusababisha watoto kukosa malezi bora na hata kuwa machokoraa mitaani na wa kike kujiuza.

Mkuu wa Dawati la Jinsia kutoka Jeshi la Polisi wilayani Shinyanga, Brightone Rutajama, aliwataka wanaume kufika kwenye dawati hilo kutoa taarifa za kufanyiwa vitendo vya ukatili na wake zao badala ya kunyamaza kwa kuhofia aibu.

Alisema kwenye dawati hilo, wanapokea malalamiko ya watu wote bila ubaguzi kisha kuyatafutia ufumbuzi ikiwamo kutatua migogoro ya ndoa. Hata hivyo, alisema wanaotoa taarifa za kufanyiwa ukatili wengi huwa wanawake.

Katika hatua nyingine, aliwataka wafanyabiashara wa stendi ya mabasi wilayani Shinyanga, bodaboda, bajaji na mawakala kuacha kufanyiana vitendo vya ukatili wa kijinsia, ikiwamo kutoleana lugha chafu za matusi ya nguoni.

Naye Mratibu wa Polisi Jamii wilayani Shinyanga, Magesa Marwa, akizungumza na madereva wa bajaji na bodaboda kwenye stendi hiyo, aliwataka kuwa mabalozi wazuri katika kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Pia aliwataka madereva hao wa bajaji na bodaboda katika msimu huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka, wazingatie sheria za usalama barabara ili kutosababisha ajali ambazo hugharimu maisha ya watu na wengine kupata ulemavu.



Rais Samia Suluhu Hassan, akikabidhi Tuzo ya Heshima ya Utatuzi wa Migogoro, Demokrasia na Haki za Binadamu kwa Waziri Mkuu mstaafu, Dk. Salim Ahmed Salim (katikati), aliyotunukiwa na Taasisi ya Kemet Butros Ghali ya nchini Misri, nyumbani kwake Masaki, mkoani Dar es Salaam jana. Anayepokea tuzo hiyo kwa niaba yake ni mtoto wake, Ahmed Salim Ahmed. **PICHA: IKULU**

# Shahidi adai kumkamata Sabaya na bastola, simu 10

**Na Allan Isack, ARUSHA**

OFISA Uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Shaban Hemed (41), amedai walimkamata aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akiwa na bastola aina ya Glock 17 ikiwa na magazini mbili zenye risasi 21.

Vilevile, shahidi huyo amedai mahakamani kuwa mbali na bastola hiyo, walimkamata mshtakiwa huyo akiwa na simu zaidi 10 na Ipad moja katika chumba ambacho alikuwa amelala.

Akisilisha ushahidi wake jana, shahidi huyo alidai walimkamata Sabaya usiku wa manane baada ya kugoma kwenda katika ofisi za taasisi hiyo kwa ajili ya kufanyiwa mahojiano.

Ofisa huyo ambaye ni shahidi wa 11 katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili Sabaya na wenzake sita, alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, Patricia Kisinda.

Mbali na Sabaya washtakiwa wengine katika shauri hilo ni Silvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Shahidi huyo alidai alihusika katika uchunguzi wa jalada la kesi hiyo ambalo lilikuwa la Sabaya kulazimisha kupewa rushwa ya Sh. milioni 90 kutoka kwa Francis Mroso.

Alidai tuhuma zilikuwa za matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji wa fedha, kujihusisha na vitendo vya rushwa, kuongoza genge la uhalifu na kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Filex Kwetukia, shahidi huyo alidai Mei 19, mwaka huu, akiwa ofisini kwake makao makuu ya TAKUKURU, majira ya mchana, bosi wake alimtaka ajiandae, kulikuwa na safari ya kwenda mikoa ya Arusha na Kilimanjaro na kwamba Mei 20, mwaka huu, akiwa na maofisa wa taasisi hiyo, waliondoka makao makuu kwenda mkoani Kilimanjaro kwa kazi hiyo.

"Uchunguzi wetu ulikuwa katika sehemu kuu mbili, ambazo ni Wilaya za Hai na Moshi, na tulichunguza taarifa fiche na kuzichakata kwa kuwahoji watu mbalimbali na baada ya hapo Mei 23 mwaka huu, tulikwenda Arusha na kutoa taarifa kwa Mkuu wa TAKUKURU Arusha na tulimweleza sababu ya kwenda na alitueleza kwamba ana jalada la tuhumu hizo ambalo lilihama kutoka polisi.

"Nanukuu maneno ya mkurugenzi alipozungumza na Sabaya kuna uchunguzi unafanyika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, hivyo anatakiwa kufika katika ofisi za mikoa hiyo, na alikubali kwenda lakini hadi kufikia Mei 24, mwaka huu, hakufika.

"Kutokana na kutompata kwenye simu Mei 25, mwaka huu, mkurugenzi alitoa kibali cha kumtafuta na kumkamata.

"Baada ya kupewa kibali cha kumkamata tulianza kukusanya taarifa za kiintelijensia kujua wapi muhusika yupo na tulibaini kwamba miongoni mwa watuhumiwa tunaowatafuta, wapo kituo Kikuu cha Polisi Arusha, ambao ni John Odemba na Daniel Mbura," alidai.

Aliendelea kudai kuwa baada ya kuwachukua watuhumiwa hao kituo cha polisi, waliwahoji na walikiri tukio na Mei 22 na walikubali kupata mgawo wa fedha zilizochukuliwa kupitia maelezo waliyoandika.

"Baada ya kutoka Arusha, tulikwenda Moshi, tulipata mwanga Sabaya anapatikana Dar es Salaam. Na nilitoa taarifa kwa bosi wangu na nilipata kibali cha kwenda kumkamata huko.

"Na kwa mujibu wa taarifa za kichunguzi walikuwa 'Beach Kindimbwi, Mtaa Kolele katika nyumba za malazi za 'MG and Home Estate'. "Tulifika chumba cha Sabaya namba 101 na 102, sikufanikiwa kuwakuta, walishatoka na baada ya kuwakosa na kujiridhisha, nilifanya mazungumzo na meneja wa apartment hizo, kama anamfahamu alikiri kuwa alikuwapo na vijana wake.

"Meneja huyo alitueleza anamfahamu Sabaya kwa kuwa alimwona katika mitandao na kijamii na alifanya malipo ya kwanza kwa simu yenye jina lake, kiasi cha Sh. 580,000, simu ambayo ilikuwa imebebwa na Silvester Nyegu na malipo ya pili yalikuwa ya Sh. 246,000, ilitumika namba ya Enock Togolani Mkeni na malipo ya tatu yalikuwa ya Sh. 968,000," alidai.

Shahidi huyo alidai kuwa baada ya kujiridhisha walikuwa wameshaondoka eneo hilo, alipitia kitabu cha kumbukumbu za magari yanayoingia na kutoka katika hoteli hiyo, akabaini walitumia gari aina ya Toyota Land Cruser V8 lenye namba za usajili T222 BDW.

Alidai kwamba kwa mujibu wa uchunguzi wao, walibaini walihamia eneo la Oasisi Village kwenye apartment ya Mount Uluguru na walipofika huko waliwakamata watu wanne katika chumba kimoja ambao ni Silvester Nyegu, Watson Mwahomange, Enock Togolani na Onjung' Saitabau na chumba kingine walimkamata Sabaya na mwanamke anayetambulika kwa jina la Jesca Thomas.

"Niliwaeleza dhumuni la kuwakamata ni kuwapeleka katika ofisi za TAKUKURU zilizoko Upanga, Dar es Salaam na walikubali kuongozana na mimi," alidai.

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, shahidi huyo alidai mahakamani huko kwamba alidai shauri hilo lilikuwa na wapelelezi wengi na kila mmoja alikuwa na nafasi yake ya kupeleleza katika kesi hiyo.

Alidai kuwa kabla ya kufika TAKUKURU, jalada hilo lilikuwa polisi kwa hatua za kiuchunguzi.

## Marekani yatoa mabilioni mradi 'Waache Wasome'

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Marekani, kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), imesherehekea miaka mitano ya mradi wa 'Waache Wasome' wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 14.75 (sawa na Sh. 33,979,520,140).

Mradi huo ulioanza Desemba 2016 hadi Februari 2022, umeongeza uandikishaji na ubakishaji wa wasichana katika elimu rasmi ya sekondari na elimu mbadala.

Hafla hiyo iliadhimisha na kuangazia mafanikio na uendelevu wa uwekezaji wa Serikali ya Marekani katika mradi wa vijana wa Waache Wasome katika kuimarisha wafanyakazi, wanafunzi na nafasi muhimu ya uwezeshaji wa wasichana katika kuboresha maendeleo ya Tanzania.

"Mtindo huu umewawezesha wasichana walio katika rika balehe kuunda na kufikia malengo ya maisha yao ya baadaye huku wakishughulikia kanuni za kijamii na vikwazo vya kiuchumi ambavyo vimezuia uwezo wao wa kubaki na kufaulu shuleni," ilisema taarifa iliyotolewa na Ubalozi wa Marekani nchini.

Mwongozo wa kuzuia Unyanyasaji wa Kijinsia Unaohusiana na Shule wa Waache Wasome (SRGBV) na mwongozo wa mafunzo ya rika wa Protect Our Youth (Linda Vijana Wetu) utatolewa na Serikali ya Tanzania kwa matumizi ya nchi nzima.

Taarifa hiyo ilisema ni hatua muhimu kwa nyenzo za mafunzo za mradi kupitishwa na serikali kwa matumizi katika shule zote. Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pia imepitisha rasmi na kuunganisha moduli ya Mfumo wa Tahadhari ya Mapema kwa wanaoacha shule (DEWS) katika Mfumo wake wa Taarifa za Shule. Shule zote za elimu ya msingi, zikiwamo za kibinafsi na za serikali, zitatumia DEWS kufuatilia na kusaidia wanafunzi walio katika hatari ya kukatisha masomo.

Waache Wasome walifikia zaidi ya wanafunzi 50,000, walimu 1,300, wazazi na walezi 6,000 katika mikoa ya Arusha na Mara. Akizungumza katika hafla hiyo, Balozi wa Marekani nchini,Dk. Donald Wright, alisifu mradi huo kwa mafanikio yake na kubainisha kuwa kuondoa vikwazo kwa elimu ya mtoto wa kike kuna manufaa mengi chanya katika jamii. "Kwa kutatua vikwazo vinavyowakabili wasichana wa Kitanzania wakiwa shuleni na katika jamii zao, wana uwezekano mkubwa wa kumaliza masomo yao. Balozi Wright pia aliipongeza Serikali ya Tanzania kwa mabadiliko ya hivi karibuni ya sera ya kuruhusu wasichana wa shule wanaopata ujauzito kuendelea na masomo..


MERES

**TAARIFA YA KUFUNGWA/ KUFUTWA KWA KAMPUNI**

Imetolewa taarifa kuwa katika mkutano wa ziada wa Meres limited namba ya usajili 130459 uliofanyika tarehe 5 Disemba 2021 azimio maalum lililo chapishwa kwa pamoja na wamiliki wa kampuni la kufunga kampuni kwani haikuweza kufanya shughuli zake, ikiwa mtu ana madai yoyote au maslahi dhidi ya kampuni wanashauriwa kuwasiliana na kampuni kwenye anwani iliyo chini ndani ya siku 7 za taarifa hii.

Mawasiliano: Sinza, Ubungo
info@meres.co.tz,0657724026,
P.O.Box 62156,Dar Es Salaam

116605702


# 'Wagonjwa msikubali kuuziwa damu ni bure'

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wametakiwa kuwaripoti wauguzi wa hospitali wanaouza damu kwa wagonjwa ili kukomesha tabia hiyo inayosababisha baadhi kupoteza maisha kwa kushindwa kununua na kudhoofisha uchangiaji damu kwa hiari.

Akitoa mafunzo kwa wahariri wa vyombo vya habari katika kampeni ya ukusanyaji damu jana jijini Dar es Salaam, Dk. Avelina Mgasa wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama, alisema kumekuwapo na malalamiko ya watu kuuziwa damu, lakini hawawaripoti wauguzi wenye tabia hiyo, hali inayosababisha kutotatua tatizo.

Mpango wa Damu Salama upo chini ya Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Dk. Mgasa alisema wananchi wanapotakiwa kununua damu ya mgonjwa wanapaswa kuripoti kwa mganga mkuu wa hospitali husika ili aweze kuchukua hatua ya kumwajibisha muuguzi huyo.

Akifafanua, Dk. Mgasa alisema mpango wa damu salama kazi yake ni kukusanya damu kwa kuhamasisha wananchi kuchangia damu kwa hiari na kuipeleka hospitali kusaidia wagonjwa bila gharama yoyote.

"Sisi tunatoa damu bure kwa hospitali zote ili wananchi wapatiwe bila kulipa, kwa sababu mwananchi hawezi kumudu gharama ya kuinunua kwa kuwa kuna gharama kubwa ya kuichakata," alisema.

Vile vile, alisema mpango wa damu salama hauwajibiki kufuatilia wagonjwa wanaouziwa damu hospitali, kwa kuwa jukumu lao ni kukusanya kuichakata na kuisambaza.

"Kama kuna malalamiko ya watu kuuziwa damu, wananchi wanapaswa kuiripoti hospitali husika ili tabia hiyo iweze kukomeshwa," alisema.

Wakitoa maoni yao kuhusu tatizo la wagonjwa kuuziwa damu, baadhi ya wahiriri akiwamo Gloria Tesha, alisema hali hiyo inadhoofisha watu kujitokeza kuchangia damu kwasababu mtu anapochangia halafu akapata tatizo na kutakiwa kununua haileti picha nzuri.

Aidha, Stella Aron, alisema baadhi ya watu wanashindwa kuripoti kwa kuhofia mgonjwa wao kutelekezwa na kupoteza maisha kwa kitendo cha kumripoti muuguzi.

Akielezea mafanikio ya Mpango wa Taifa wa Damu Salama, Dk. Wilhelmus Mauka, alisema kwa mwaka 2021/2022 Mpango umeweka malengo ya kukusanya chupa za damu 375,000 sawa na asilimia 75 ya mahitaji ya damu nchini ambayo ni 550,000.

Dk. Mauka alisema kumekuwa na ongezeko la makusanyo ya damu kila mwaka na mpaka kufikia mwaka wa fedha wa 2020/2021 damu salama ilikusanya jumla ya chupa za damu 331,279, ikilinganishwa na chupa 12,597 zilizokusanywa kwa 2005 wakati mpango huo unaanzishwa.

Vilevile, alisema timu za uhamasishaji, ukusanyaji damu zimeongezeka kutoka saba mwaka 2015 hadi kufikia 286.

Dk. Mauka alisema kwa upande wa Bara asilimia zaidi ya 60 zinakusanywa na timu za halmashauri.

# Butiku asema Katiba ni jambo la lazima

**Na Thobias Mwanakatwe**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere na mwanasiasa mkonge nchini, Joseph Butiku, amesema kuiboresha katiba na hata kuiandika upya ni jambo la lazima.

Alisema hayo juzi akihojiwa kwenye kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na runinga ya ITV kuhusu tathmini ya hali ilivyokuwa baada ya Tanganyika kupata uhuru na hali ilivyo sasa miaka 60 baada ya uhuru.

Butiku alisema suala la marekebisho ya katiba haliepukiki. "Mimi nasema katiba ni muhimu kuiboresha, ni lazima na hata mkitaka mpya ni lazima, hii katiba tuliyonayo iliboreshwa tu wala mambo yake hayakuwa mengi, iliboreshwa katika mambo ya madaraka ya Rais na madaraka ya wabunge na haki za wananchi," alisema Butiku.

Hata hivyo, alisema Watanzania wawe na tabia ya kutii kwani Rais Samia Suluhu Hassan alishasema suala la katiba ni muhimu, lakini apewe muda kwanza ashughulike na suala la kuboresha uchumi wa nchi.

"Tunaye Rais, anasema ni jambo jema, lakini tujipe muda tushughulike na uchumi wetu, mimi nadhani tujenge tabia ya utii na kusikiliza, itafika mahali kama Rais Kikwete alivyoona... Rais huyu wa sasa au mwingine ataona, katiba na yaliyomo inajipima vizuri katika matendo sio katika kelele ya kudai."

"Ni lazima tukubali nafasi ya uhuru wa kuzungumzia katiba yetu na tukitaka kuibadili tuwe huru kuzungumza na vile vile tuwe taifa ambalo tuna mwafaka wa kufanya hivyo kwani turijaribu tukaishia njiani.



"Kwanza katiba tunayo, wanaotaka sana sababu zao, ipo katiba mpya imetengenezwa tunayoitwa katiba pendekezwa ila haikwenda kwenye stage (hatua) ile ya mwisho kwamba iende kwa wananchi waipigie kura tuseme hii ndio katiba yetu," alisema Butiku.

Butiku alisema katiba pendekezwa ilipitishwa na Bunge Maalum la Katiba baada ya kufanyiwa kazi na tume iliyoteuliwa kikatiba na kwa mujibu wa sheria, na kwamba hiyo kazi ilishafanyika.

"Kikubwa zaidi muwe tayari kujenga tabia ya kutekeleza na kutii yale yaliyomo katika katiba, kama mnaandika kitabu halafu hamtekelezi kwanini mnataka kuandika vitabu vipya? Alihoji.

Alisema katika katiba kuna misingi na utaratibu kwa ajili ya utendaji, hivyo viongozi na wananchi lazima wakubali kutenda kwa mujibu wa katiba na kama hawatAweza kufaulu hayo hakuna sababu ya kuwa na katiba mpya.

"Mnataka katiba ya vyeo au mnataka katiba ya kuwatafutia kazi, kama ni katiba ya kusaidia kuimarisha misingi yetu ya maisha ambayo inatambua utu wetu na haki zetu zote na maisha bora kwa kila mtu... katiba hii tuliyonayo hatujaanza kutekeleza ipasavyo," alisema.

**VYAMA VYA SIASA**

Akizungumzia kuhusu vyama vya siasa kama vinafanya siasa inayokidhi mahitaji ya wananchi kwa wakati huu, alisema vinajitahidi kwasababu vinatambua kuwa kuna siku vinakwenda kuwaomba wananchi kura japo viongozi wanatumia muda mwingi kubishana kuhusu nafasi zao.

"Sina uhakika kama wanatumia muda mwingi leo kushughulikia maendeleo na hali za wananchi, naona kama wanatumia muda mwingi kubishana kuhusu nafasi zao, nani atakuwa rais, nani atakuwa hiki," alisema.

Butiku aliongeza kuwa kutokana na mabishano hayo yaliyopo ndani ya vyama ndio maana wakati wa uchaguzi kunakuwa na vurugu wakati wote na huwezi kujua lini uchaguzi umekwisha na lini tuendelee na kazi ya maendeleo na watu wawape nafasi ya kuwapima kama kweli wanashughulika na mambo yako," alisema.

Kuhusu mfumo wa vyama vingi vya siasa alisema bado haujaeleweka kwa wananchi na viongozi wa vyama vya siasa.

"Viongozi wa vyama wengi hawajaelewa kwamba mifumo hii sio ugomvi, mifumo hii ni ya kukoleza utaratibu wa kujadili namna ya kusaidiana na wananchi wakishiriki katika mazungumzo hayo hasa jinsi ya kuendesha nchi," alisema.

# 'Malkia wa Tembo' ahukumiwa upya

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imemhukumu upya kifungo cha miaka 9 jela malkia wa meno ya tembo, Yang Feng Glan na wenzake wawili baada ya kuwatia hatiani kwa makosa matatu ya kujihusisha na biashara haramu ya meno ya tembo yenye thamani ya Sh. bilioni 13.9.

Washtakiwa hao walihukumiwa kwa mara ya kwanza na kupewa adhabu ya miaka 15 jela kuanzia Februari mwaka 2019, Mahakama Kuu ilifuta adhabu na kuamuru jalada kurudi Mahakama ya Kisutu kwa kuandika hukumu upya ambapo jana walisomewa hukumu yao.

Mbali na Malkia wa meno ya tembo, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi ni Salvius Matembo na Philemon Manase.

Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi alisema hukumu dhidi ya washtakiwa hao ilishatoa mwaka 2019, walikata rufani Mahakama Kuu ambapo katika uamuzi wake iliamuru jalada lirejee Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Alisema Mahakama Kuu ilielekeza hukumu iandikwe upya na ielezwe washtakiwa walitiwa hatiani kwa makosa gani.

"Washtakiwa walikuwa wakikabiliwa na mashtaka matatu, kujihusisha na mtandao wa uhalifu makosa mawili na kujihusisha na biashara haramu ya meno ya tembo.

"Hoja iliyopo kuangalia je, washtakiwa wanajuana? Kutokana na ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri imethibitika kwamba washtakiwa wanajuana.

"Mashahidi walielezea mshtakiwa wa kwanza na wapili walivyofahamiana katika biashara ya meno ya tembo, ilionyesha walikuwa wanakusanya na kupeleka kwa malkia.

"Mshtakiwa watatu, Malkia ushahidi ulionyesha alipokea, alipima na kuficha na kati ya mshtakiwa wa kwanza na wapili kulikuwa na miamala ya kutumiana fedha, walishindwa kueleza fedha hizo zilikuwa za nini," alisema Hakimu Shaidi.

Alisema kuhusu kufahamiana, ushahidi umebainisha kuwa walikuwa wanafahamiana washtakiwa wote watatu.

"Mahakama imejiridhisha kwamba makosa yalithibitika bila kuacha shaka yoyote, Mahakama inamtia hatiani mshtakiwa wa tatu Malkia kwa kosa la kujihusisha na genge la uhalifu, inawatia hatiani mshtakiwa wa kwanza na wapili kwa kosa la kujihusisha na genge la uhalifu na inawatia hatiani washtakiwa wote kwa kosa la kujihusisha na biashara ya meno ya tembo," alisema.

Baada ya washtakiwa kutiwa hatiani, Wakili Nehemiah Nkoko aliomba mahakama iwapunguzie adhabu kwa kuzingatia tayari walishatiwa hatiani, walianza kutumikia kifungo kabla ya Mahakama Kuu kufuta adhabu hiyo.

Alidai Mahakama Kuu ilisema washtakiwa walikaa gerezani miaka sita, lakini kwa kuangalia mwaka wakioshtakiwa 2014, walikaa miaka zaidi ya saba.

Wakili Nehemiah alidai Malkia kwa sasa ana miaka 70 na mgonjwa, hivyo aliomba apunguziwe adhabu kutokana na umri wake mkubwa.

Wakili wa Serikali, Faraja Nguka, aliomba pamoja na kupewa adhabu inayostahili, shamba la Malkia lililopo Muheza Tanga litaifishwe na kuwa mali ya serikali.

Akitoa adhabu Hakimu Shaidi alisema alizingatia hoja za pande zote mbili, ni kweli walikaa gerezani muda mrefu, walianza kutumikia kifungo kabla ya Mahakama Kuu haijatoa hukumu.

"Mliwakosea Watanzania wote, mliua au kusababisha tembo wengi kuuawa, tembo ni chanzo cha mapato ya fedha za kigeni, mshtakiwa wa kwanza na wapili ni Watanzania, lakini mliamua kujinufaisha wenyewe.

"Mshtakiwa watatu, wewe ni raia wa kigeni ulikaribishwa na uliamua kufanya ulichofanya kana kwamba nchi ilikosea kukukaribisha, chezeni mziki wenu, mlioupiga wenyewe," alisema Hakimu Shaidi.

Baada ya kusema hayo alitoa adhabu, kwa kosa la kwanza la kujihusisha na genge la uhalifu Malkia atakwenda jela miaka 15, kosa la pili kama hilo, washtakiwa wawili waliobakia watakwenda jela miaka 15.

Katika kosa la tatu washtakiwa wote watalipa faini mara mbili ya thamani ya meno ya tembo Sh. bilioni 13.9 ambayo ni sawa na Sh. bilioni 27.8, endapo watashindwa watakwenda jela miaka miwili na adhabu zinakwenda kwa pamoja.

Alisema Mahakama inatoa amri ya kutaifisha shamba la malkia lililoko Muheza Tanga kuwa mali ya serikali.

Washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo kati ya Januari mosi na Mei 22, mwaka 2000, maeneo mbalimbali nchini.

Wanadaiwa kujihusisha na biashara haramu ya meno ya tembo 860 ambayo ni sawa na tembo 430 yenye kilo 15,900 bila kuwa na kibali.

Mahakama imepunguza miaka sita kutoka 15 ambayo hakimu huyo, aliwahukumu jana kabla ya kupunguza, hivyo kuwa miaka tisa imezingatia ukweli kwamba walikaa muda mrefu gerezani miaka sita.



Balozi wa Qatar nchini Tanzania, Hussain Ahmad Al-Homaid (katikati), akikata utepe kuzindua ofisi za taasisi ya kutoa msaada ya Qatar Charity, Masaki, mkoani Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Jassim Al Jassin na (kushoto) ni Meneja Mkaazi wa taasisi hiyo, Mhandisi Omar Saleh. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Taharuki ujambazi yatikisa D'Salaam

**Na Elizabeth Zaya**

TAHARUKI miongoni mwa wakazi wanaoendesha shughuli zao katika eneo la Lumumba, Ilala jijini Dar es Salaam ilizuka jana baada ya eneo hilo kudaiwa kuvamiwa na watu waliodhaniwa majambazi.

Watu hao walidaiwa kuvamia moja ya nyumba za ghorofa katika mtaa huo wa Lumumba majira ya saa tano asubuhi mpaka saa sita mchana.

Baadhi ya mashuhuda wa taharuki hiyo walidai kuwa baada ya watu hao waliodhaniwa kuwa majambazi kuvamia, askari wa Jeshi la Polisi walifika na kuzingira eneo hilo huku wakirusha risasi.

Baadhi ya picha za video za tukio hilo zilizosambazwa kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha askari wakiwa wamezingira eneo hilo wakiwa na silaha za moto.

Hata hivyo, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema jana kuwa tukio hilo halikuwa la ujambazi bali vijana wawili ambao siyo wenyeji katika eneo hilo, walipanda ghorofani na hivyo wenyeji kushtuka na kuzua taharuki hiyo.

"Siyo majambazi, bali kuna vijana wawili ambao siyo wenyeji walipanda katika ghorofa hilo, na wakiwa huko, mwanamke mmoja anayeishi hapo aliwaona na hivyo akashtuka na kupiga kelele, akiomba msaada na vijana hao wakakimbia," alisema Muliro.

"Kwa hiyo baada ya kelele hizo, mkazi mwingine anayeishi katika ghorofa hilo aliyejulikana kwa jina la Amour Juma ambaye ni raia mwema, alifyatua risasi tatu hewani na alifanya hivyo baada ya kusikia kelele kuomba msaada," alisema.

Kamanda Muliro alisema tukio hilo lilitokea majira ya saa tano asubuhi mpaka saa sita mchana katika jengo lenye ghorofa zaidi ya sita lenye mchanganyiko wa watu wengi.

"Kimsingi hakuna ujambazi uliofanyika eneo lile licha ya kufyatulia risasi hizo tatu kutoka kwa mtu anayemiliki silaha kihalali.

"Uchunguzi unafanyika kujua wale vijana walikuwa kinanani, nia yao ilikuwa ni nini na kimsingi hawakuwa na bunduki wala panga licha ya kwamba walifika na kuingia mpaka juu ghorofani kwenye eneo hilo," alifafanua.

# Kampeni matumizi ya mashine EFD yarindima

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mapato (TRA) imeanza kampeni ya kuhamasisha matumizi ya mashine za kielektroniki za kutolea risiti (EFD) na kuwahimiza wanunuzi kudai na kukagua risiti kila wanaponunua bidhaa na huduma mbalimbali.

Akizungumza wakati wa kampeni hiyo iliyoanzia Kariakoo, Msimamizi wa Kitengo cha EFD wa Mkoa wa Kikodi Kariakoo, Hamidu Shaban, alisema jana kuwa kampeni hiyo ni endelevu na inafanyika katika maeneo yote ya Dar es Salaam.

"Tunafanya zoezi hili katika mkoa mzima wa Dar es Salaam kwa kuhakikisha wafanyabiashara wanatoa risiti kuanzia kwenye mizigo yote inayozalishwa viwandani na kupelekwa madukani, inauzwa kwa risiti na kuhakikisha wale wanaonunua bidhaa wanadai risiti," alisema Shaban.

Alizitaja adhabu za kutokutoa na kudai risiti kuwa ni faini ya Sh. milioni 1.5 hadi milioni 4.5 kwa wafanyabiashara wasiotoa risiti za EFD na wanunuzi wasiodai risiti adhabu ni Sh. 30,000 hadi milioni 1.5.

Rehema Mbilinyi, mfanyabiashara wa Kariakoo, alibainisha kufurahishwa na kampeni hiyo ya kuhamasisha matumizi ya EFD, akiiomba serikali kugawa makundi ya wafanyabiashara wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa kuweka viwango tofauti vya kodi ili kuondoa tatizo la baadhi ya wafanyabiashara kutoa risiti pungufu au kutokutoa kabisa kwa kuogopa kuingia kwenye VAT.

"Kampeni hii ni nzuri lakini mimi ninaona kuna haja ya serikali kutoza kodi ya VAT kwa kugawa makundi. Kwa mfano, wale wafanyabiashara wakubwa wawe na asilimia 18 kama kawaida, wafanyabiashara wa kati watozwe asilimia 10 na wasajiliwa wapya wa VAT waanze kwa asilimia tano.

"Hii itasaidia kupunguza tatizo la kutokutoa risiti au kutoa risiti pungufu," Rehema aliwasilisha ushauri wake huo kwa TRA.

Sylivanus Nyigu, mfanyabiashara wa Kariakoo, mbali na kuipongeza TRA kwa kampeni hiyo, alisema elimu hiyo itasaidia kuondoa upungufu unaojitokeza kwenye kutoa na kudai risiti na kuutafutia ufumbuzi.

TRA imekuwa na utaratibu wa kufanya kampeni za mara kwa mara kwa lengo la kuwaelimisha wafanyabiashara kuhusu masuala yanayohusu kodi, kuhamasisha matumizi sahihi ya mashine za EFD pamoja na kuwakumbusha walipakodi kulipa kodi kwa wakati.

# Matangazo tiba asili yapigwa marufuku

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA la Tiba Asili na Tiba Mbadala limepiga marufuku matangazo yote ya tiba asili na tiba mbadala katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Vilevile, baraza hilo limezuia uuzaji wa dawa za tiba asili na tiba mbadala kiholela kwenye vyombo vya usafiri, nyumba za ibada na sokoni.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Prof. Hamisi Malebo, alitangaza uamuzi huo jana jijini hapa alipotoa tamko la baraza kuhusu usajili wa dawa, waganga wa tiba asili na tiba mbadala pamoja na vibali vya matangazo.

"Matangazo yote ya tiba asili na tiba mbadala ni lazima yapate kibali cha baraza kabla ya kurushwa katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

"Hivyo, matangazo yote ambayo hayakupitishwa na baraza yamesitishwa kuanzia leo, kwa pamoja tuhakikishe huduma zote zinatolewa kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo," alisema.

Prof. Malebo pia aliwataka waganga wote ambao wanatoa huduma bila usajili, kila mmoja kukamilisha usajili wake ifikapo Machi 31, mwakani.

"Tunatoa miezi mitatu ya msamaha kwa wote ambao bado hawajafanya usajili, baada ya hapo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao ikiwa ni pamoja na kuwafikisha katika vyombo vya sheria," alionya.

Pia aliwataka waganga wote kujiepusha na vitendo vinavyokinzana na sheria, kanuni na taratibu zilizopo, ikiwa ni pamoja na kuacha mara moja tabia ya kuweka mabango yenye ujumbe unaopotosha jamii.

"Kurusha matangazo kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii bila kupata kibali kutoka baraza, kuuza dawa kiholela kwenye vyombo vya usafiri, nyumba za ibada na sokoni, dawa zote zitauzwa katika maduka ya dawa za asili yaliyosajiliwa," alisema.

Alikumbusha kuwa ni kosa na hairuhusiwi kuhusisha tiba asili na uchawi au mambo yote ya kishirikina kama vile upigaji ramli, matumizi ya viungo vya binadamu katika tiba, mauaji ya wenye ualbino, mauaji ya vikongwe na kufichua wachawi, maarufu lambalamba.

"Napenda kuwakumbusha kuwa ni marufuku kutumia mashine za Quantum pamoja na zile zinazodaiwa kutoa sumu mwilini, utakapokutwa na vifaa hivyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yako," alisema.

Alisema usajili wa waganga ulianza rasmi mwaka 2010 na hadi kufikia Novemba 30, 2021 waganga 29,459, vituo 1,077, dawa za asili 67 zilikuwa zimesajiliwa na baraza hilo.

## AFF, SUA zaandaa mwongozo tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

JUKWAA la Misitu Afrika (AFF) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), wameandaa mwongozo maalum wa kufundisha kozi fupi za mabadiliko ya tabia nchi kwenye misitu.

Akizungumza juzi wakati wa ufunguzi wa mkutano wa wataalamu na wadau wa misitu wa nchi za Cameroon, Uganda, Kenya, Msumbiji, Tanzania, Zambia na Zimbabwe, Katibu Mtendaji wa Jukwaa hilo, Prof. Godwin Kowero, alisema mwongozo huo utahusisha maeneo manane muhimu.

Aliyataja maeneo hayo kuwa ni mafunzo ya sayansi ya awali ya mabadiliko ya tabia nchi kwa wanataaluma, kiufundi, misitu ya Afrika, soko na biashara ya kaboni kwa wananchi na wataalamu, mifano ya hali ya hewa na maendeleo, mijadala ya kimataifa na mchakato wa kusukuma mbele hoja za nchi duniani, pamoja na mbinu mbalimbali.

"Mwongozo huu wa mafunzo umetafsiriwa pia kwa lugha ya Kifaransa. Zaidi umejikita kwenye maeneo matatu ya kukabiliana na mawili ya kupunguza mabadiliko ya tabia nchi kwenye misitu, tupo hatua ya mwisho ya kukamilisha mwongozo wa kupunguza mabadiliko ya tabia nchi kwenye misitu kwa ajili ya wanataaluma," alisema.

Kwa mujibu wa Prof. Kowero, matarajio ni kuwa mwongozo huo utaleta mabadiliko ya namna elimu na mafunzo yanatolewa na vyuo vikuu vingi Afrika, vyuo vya kati na taasisi za ufundi kuhusu mabadiliko ya tabia nchi kwenye misitu.

"Tunaamini mwongozo huu wa kozi fupi utakuwa ufunguo wa haraka kuwajengea uwezo makundi mbalimbali kwenye mabadiliko ya tabianchi kwenye misitu kwa mashirika yasiyo ya kiserikali, wataalamu wa ugani wa misitu na wafanyakazi kwenye taasisi za elimu na utafiti ambao hawajapata uelewa wa jambo hili," alibainisha.

Akiwasilisha mwongozo huo kwa washiriki wa mkutano huo, Katibu Mkuu wa AFF, Prof. Marie Louise Avana, alisema kila somo litakuwa na matokeo maalum ya namna ya kutunza misitu na kupunguza mabadiliko ya tabianchi kwenye misitu ambayo ni muhimu kwa maisha ya watu, viumbe na maendeleo.

Mathalani, alisema katika mafunzo ya biashara na masoko ya kaboni, watakuwa na uelewa na kuchambua mbinu, uhusiano wake na kuuza mazao ya misitu, kutambua rushwa na mambo yaliyo kinyume cha sheria kwenye biashara hiyo.

Kwa mujibu wa Prof. Avana, mwongozo huo utasambazwa kwa nchi zote zinazozungumza Kiingereza na Kifaransa na lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo washiriki wanaofanyakazi na jamii waiwezesha jamii kutambua fursa zilizopo kwenye misitu, sera, mipango na shughuli mbalimbali.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA SHUGHULI ZA MAZINGIRA KATIKA MRADI WA EACOP TANZANIA. KUMBUKUMBU:10007246**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V. inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya shughuli za mazingira katika mradi wa EACOP Tanzania.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

Miundo mbinu itakayojengwa juu ya ardhi kwa Tanzania itahusisha vituo 4 vya pampu, vituo 2 vya kupunguzia kasi ya mtiririko wa mafuta; kituo kikuu cha kuhifadhia mafuta karibu na bahari (Marine Storage Tank) na kituo cha kupakilia mafuta (Load Out Facility); kambi 12 za wafanyakazi na kuhifadhia mabomba, barabara za kuelekea kwenye vituo na makambi; na vituo vya kuvunia mwanga wa jua (solar farms).

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

Mradi wa EACOP unahitaji watoa huduma wenye uzoefu na uwezo yakinifu wa kutoa huduma za shughuli za mazingira katika mawanda mbalimbali ya mradi ambayo yatahusisha:

- Tathmini ya athari za mazingira na jamiii pamoja na kuandaa taarifa za madhara hayo.
- Utafiti wa taarifa za msingi za mazingira-nchi kavu na baharini.
- Kutengeneza na kuwasilisha mpango mbadala wa bioanuai pamoja na tathmini na usimamizi wa pamoja wa huduma za mfumo wa ikolojia wa nchi kavu na baharini, ukusanyaji wa taarifa na maendeleo ya mkakati wa usimamizi.
- Kutengeneza na kutekeleza programu za kutunza na kuhifadhi mali asili za kijamii.
- Ufuatiliaji na uthibiti wa taarifa za mazingira kufuatana na sheria zilizopo.
- Kuandaa leseni na vibali vya mazingira.
- Huduma ya kuwasilisha taarifa za mazingira.
- Ukaguzi wa kuangalia utaratibu na utekelezaji wa sheria za mazingira.
- Ushauri wa jumla kuhusu mada mbalimbali za mazingira.

**VIGEZO MUHIMU:**

- Uthibitisho wa uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi za huduma za kimazingira katika mawanda ya kazi, kwa viwango vya juu nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 5 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa watendakazi husika wenye vigezo na uzoefu wa hali ya juu katika kufanya tathmini ya athari za mazingira na jamiii pamoja na kuandaa taarifa za madhara hayo katika miradi ya mafuta na gesi.
- Uzoefu wa kufanya tathmini ya athari za mazingira na jamiii ambao unakidhi vigezo na mahitaji ya IFC and EP IV.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma inayotakiwa ikihusishwa na mawasilisho ya taarifa ya kifedha (financial accounts) kwa Mwaka 2020.
- Inashauriwa, muonesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa sera ya ndani ya Ubora, Afya, usalama na Mazingira, taratibu na mchakato kulingana na viwango vya ndani vya viwanda vya kazi husika.
- Uthibitisho wa usajili katika mamlaka husika ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma husika.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacoptz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11** jioni za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **20 Disemba 2021.** Kichwa cha barua pepe kiwe ni **10007246.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mawaziri wazibane bodi za mashirika ya umma

**KUFANIKIWA** au kufeli kwa mashirika au taasisi za umma katika utendaji wa majukumu yake kwa kiwango kikubwa ni matokeo ya namna gani bodi za wakurugenzi zinavyosimamia.

Mchango wa bodi hata kwa uendeshaji wa kampuni au shirika binafsi ni mkubwa, kwa kuwa bodi ndizo zinazopanga/kuweka malengo ya kutekelezwa na menejimenti (uongozi), kufuatilia utekelezaji wake na mwishowe kupima matokeo kama malengo yaliyowekwa yametekelezwa.

Kwa majukumu zilizonayo bodi tunaweza kuona kwamba ndizo zenye wajibu katika kuhakikisha kwamba mashirika na taasisi yanafikia malengo kwa tija na ufanisi, kinyume chake bodi zinapaswa kuwajibika.

Ndiyo maana pale shirika au kampuni inapofanya vibaya katika utendaji, bodi inakuwa ya kwanza kuwajibika au kuwajibishwa, ikiwamo kuvunjwa.

Tumeshuhudia mashirika na taasisi nyingi za umma zikifeli katika utekelezaji wa majukumu yake na matokeo yake ni kuisababishia hasara serikali. Matukio haya mara nyingi yamekuwa yakihusishwa na bodi kushindwa kuwajibika katika usimamizi.

Kwa bahati mbaya sana pamoja na mashirika yetu kadhaa ya umma kutofanya vizuri na mengine kufa na kuiachia serikali madeni ya mabilioni pamoja na hasara, chanzo chake hakielezwi wala wajumbe wa bodi hawachukuliwi hatua za kisheria zaidi ya bodi kuvunjwa.

Tunampongeza sana Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, kwa ujasiri wake wa kuliweka sawa jambo hili. Juzi Prof. Mbarawa alifichua jinsi gani wajumbe wa bodi wanavyochangia utendaji mbovu wa mashirika ya umma kutokana na kutowajibika katika kutanguliza maslahi ya umma.

Akizindua Bodi mpya ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), juzi jijini Dar es Salaam, Prof. Mbarawa alisema bodi za mashirika hayo yanapaswa kutanguliza maslahi binafsi na kwamba ndio maana nyingi zinavunjwa kutokana na kushindwa kusimamia ununuzi, maslahi binafsi pamoja na kuendekeza urafiki.

Kwamba nyingi zinashindwa kutimiza majukumu ziliyopewa kutokana na baadhi ya maofisa watendaji wakuu wa mashirika 'kuwashika' wajumbe wa bodi, hali inayosababisha kila jambo wanalopelekewa kulipitisha pasipo kuhoji.

Alisema wajumbe wa bodi wengi wanakuwa na maslahi binafsi, hali inayowasababishia kujisahau kutimiza majukumu waliyopewa.

Kwa mujibu wa utaratibu, mwenye mamlaka ya kuteua wenyeviti wa bodi za taasisi na mashirika ya umma ni Rais, huku waziri husika akiwa na mamlaka ya kuteua wajumbe. Kwa misingi hiyo, tunaona kwamba mawaziri wana wajibu wa kusimamia na kuzifuatilia kwa bodi kama zinatimiza wajibu wake sawasawa na inavyotakiwa. Alichokisema Waziri Mbarawa ndicho kinachoendelea katika mashirika mengi, kutokana na watendaji wakuu 'kuwashika' wajumbe kwa maana ya kuwapa 'bahasha' na takrima nyingine nyingi ambazo ni kinyume cha utaratibu ili wasifurukute.


Alichokisema Prof. Mbarawa kinaakisi uhalisia wa hali ilivyo kwenye mashirika hayo. Itakumbukwa jinsi baadhi ya mashirika katika miaka ya nyuma yalivyokuwa yakipeleka mikutano ya bodi kufanyikia Afrika Kusini, Dubai na nchi zingine, hivyo kuigharimu nchi mabilioni ya shilingi!

Pamoja na Rais kuwa ndiye mwenye mamlaka ya kuzivunja bodi, tunaona kwamba njia pekee ya kuyanusuru mashirika yetu na taasisi ni mawaziri husika kuwa wakali na kumshauri Rais kuzivunja bodi inapobainika utendaji unayumba.

Ili wajumbe kuwafanya wajumbe wa bodi wawajibike kulinda na kutanguliza mbele maslahi ya umma, serikali ifikirie pia kuweka taratibu za kuwawajibisha kisheria pale wanapobainika kuzembea au kuhusika katika kuisababishia nchi hasara.

Pia tunaona kuwapo haja ya kubadili mitazamo katika uteuzi wa wajumbe wa bodi zetu kwa kuangalia uwezo wa wajumbe ukiwamo ubunifu badala ya kuteua watu kwa ajili ya kuwapa zawadi hata kama umri umewatupa mkono au kuwapa shukrani, vinginevyo hakutakuwapo na tija wala ufanisi katika utendaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Miaka 60 ya Uhuru na kazi ziendelee

**MIONGONI** mwa sifa ambazo Tanzania inapata katika miaka ya mwanzo ya uhuru, ni kwenye diplomasia ya ukombozi Kusini mwa Afrika hatua hiyo ikihusisha mikakati ya kushawishi kuwapo na mtangamano wa Afrika.

Wakati huo Mwalimu Julius Nyerere, akijikita kuendeleza mshikamano, kutatua migogoro katika nchi hizo na kusimamia sera zake za nje na kufanikiwa kuzifanya kuwa karibu.

Tanzania inapotimiza miaka 60 ya uhuru, ina mengi iliyofanya hata nje ya mipaka, ikiwamo kuhifadhi wapigania uhuru na kuongoza mapambano ya uhuru Kusini mwa Afrika; Msumbiji, Afrika Kusini, Zambia, Zimbabwe na Namibia na Angola.

Si hapo tu, bali pia imepigania umoja wa Afrika kwa kuanza na mtangamano wa kikanda kama kuanzishwa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na pia kurejesha Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) iliyovunjika mwaka 1977.

Pamoja na hayo, katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru, Tanzania imepokea na kuhifadhi wakimbizi kutoka mataifa jirani ambao nchi zao zimekumbwa na migogoro na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Kesho Watanzania watakuwa wanahitimisha kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru wa nchi yao, uliopatikana Desemba 9, mwaka 1961, wakiwa wamoja na wenye kuvumiliana katika mambo mbalimbali kama itikadi tofauti za kisiasa.

Hali hiyo inatokana na misingi ya amani ambayo imekuwapo kabla na baada ya uhuru, ambayo imesimamiwa na viongozi waliopita na sasa inaendelezwa na waliopo madarakani kwa manufaa ya Watanzania.

Lakini, Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizopokea mageuzi ya kisiasa mwaka 1992 na inayaendeleza kwa amani ingawa zipo kasoro kadhaa zinazolalamikiwa na vyama vya upinzani.

Pamoja na kuwapo kwa kosoro bado kumekuwapo na umoja, huku viongozi wa vyama hivyo wakitafuta zaidi kuwapo kwa meza ya mazungumzo ili kupata muafaka kumaliza tofauti.

Wakati huu ambao nchi inaadhimisha miaka 60 ya uhuru, ni vyema kuendelea kuwa na utaratibu wa majadiliano ili kuapata mufaka kwa njia ya mazungumzo ambao kimsingi unaendelea kuwafanya Watanzania kuwa wamoja.

Wakati wa kusherehekea uhuru pale panapohitajika kuongeza kasi kwa ajili ya kumaliza malalamiko ya kisiasa au kero za Muungano, basi ingependeza kama itaongezwa ili kuendelea kuimarisha umoja wa Watanzania wote.

Kwa kuwa nchi imetimiza miaka 60 huku watu wake wakiwa wamoja, basi si vibaya kama kasoro ndogo ndogo ambazo zimekuwa zikilalamikiwa kwenye siasa na hata katika muungano zikafanyiwa kazi.

Ninaamini kwamba, kila Mtanzania kwa nafasi yake, ana mchango katika kuhakikisha mambo ambayo anadhani yanaweza kusababisha umoja ukasambaratika yanapatiwa ufumbuzi.

Kila mmoja anaweza kushirikiana na viongozi wa umma kwa kutoa ushauri au mchango wa kumaliza tofauti za kisiasa kati ya vyama vya upinzani na serikali, kutokana na kwamba wote wanajenga nyumba moja ambayo ni Tanzania. Hivyo, kwa hali hiyo haina haja kugombea fito na kusababisha kutokuwapo kwa umoja ambao umedumu kwa miaka 60 ya uhuru sasa bila kuwapo vurugu za kisiasa.

Kama ambavyo nchi ilipokea mageuzi ya kisiasa bila vurugu, ni vyema kuyaendelezwa, na ndivyo hata katika suala la muungano kama ambavyo umewafanya Watanzania kuwa wamoja, nao uendelee kuimarishwa.

Jambo la muhimu katika kufanikisha hayo yote ni kila mmoja kufanya sehemu yake kwa kuepuka kugawanywa kwa tofauti za kisiasa au kwa namna yoyote ile inayoweza kusababisha watu kutokuwa wamoja.

## Diwani aonya mikopo umiza

**Na Julieth Mkireri**, KIBAHA

WAKAZI wa Kata ya Tumbi Wilaya ya Kibaha wametakiwa kujiridhisha na riba kutoka kwenye taasisi zinazotoa mikopo ili kuondoa usumbufu unaoweza kutokea pindi wakishindwa kurejesha kwa wakati.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana mjini hapa na Diwani wa Tumbi, Raymond Chokala, alipokuwa akifungua mafunzo kwa wajasiriamali ambayo yameandaliwa na Shirika la Elimu Kibaha kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji Kibaha.

Chokala alisema ziko baadhi ya taasisi badala ya kuwa mkombozi zinekuwa zikichangia kudidimiza wajasiriamali kutokana na riba walizo nazo.

"Kabla ya kukopa tujiridhishe kama utamudu riba. Wako ambao wakikwama kurejesha na vitu vyao vinachukuliwa hali ambayo inawarudisha nyuma," alisema.

Pia alizitaka serikali za mitaa kufuatilia taasisi za fedha zinazotoa mikopo kwenye maeneo yao ili kuepuka kuruhusu zenye riba kandamizi kutoa mikopo kwa wananchi ambao baadaye wanaathirika.

Katika hatua nyingine, Diwani huyo alitoa wito kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kufikisha elimu kwa wananchi hususani wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ili kukata bima na kuondokana na adha wanayokumbana nayo kwa sasa wanapohitaji huduma za afya kipindi ambacho hawana fedha.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara wadogo (machinga) Mkoa wa Pwani, Philemon Maliga, aliishukuru serikali kwa kuwatengea maeneo ya biashara.

Maliga alisema awali walikuwa wanafanyabiashara kila mmoja na eneo lake ambalo sio rasmi hali ambayo ilikuwa kikwazo kwao kupata mikopo fursa zinapotokea kutokana na kutokuwa na maeneo maalumu.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Tumbi, Clara Mwingira, alisema katika mwaka wa fedha 2020/2021 vikundi 25 vya kata hiyo vimenufaika na mikopo inayotolewa na halmashauri.

# Kamanda atangazia kiama wanaofanyia ukatili watoto

**Na Elizabeth Zaya**

KAMANDA wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, amewatangazia kiama wale wote watakaobainika kuwafanyia ukatili watoto katika mkoa huo.

Kamanda Muliro alisema hayo jana alipokaribishwa kuwa mgeni rasmi katika kongamano la kujadili namna ya kukomesha vitendo vya ukatili lililoandaliwa na Kituo cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake na Watoto (WLAC) ikiwa ni mwendelezo wa Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

Alisema pamoja na jitihada zinazofanywa na wadau mbalimbali wakiwamo WLAC, wanasheria na Jeshi la Polisi kupambana na vitendo hivyo, bado vinaendelea kufanywa hususani kwa watoto.

"Tumeshuhudia juhudi kubwa zinazofanywa na wadau mbalimbali, WLAC, wanasheria, Jeshi la Polisi nalo kupitia dawati la jinsia, wamekuwa wakielimisha sana na kupambana na vitendo hivi vya ukatili hasa vinavyoendelea kufanywa kwa watoto, lakini bado hawasikii wanaendelea kushupaza shingo na kuwakatili watoto hawa, sasa mimi nasema hivi, niko tayari kumtia mtu kwenye tanuri la kisheria, yeyote anayendelea kuendekeza vitendo hivi, hatabaki salama," alisema Muliro.

"Si wakati wa kuoneana huruma tena kwa sababu watu hawa wanatuharibia watoto na ambao ndiyo viongozi wajao, wanatengeneza taifa ambalo limeharibiwa na kwa namna hii siko tayari kuendelea kuvumilia wahalifu wa namna hii kama ambavyo sijawahi kumvumilia mhalifu yeyote, lazima wakutane na tanuri la sheria na nitasimamia kwa nguvu zote muongozo wa kisheria kuhakikisha kwamba wanawajibishwa."

Aliwaomba wananchi kushirikiana na jeshi hilo katika kuwabaini watuhumiwa wanaofanya vitendo hivyo vya ukatili kwa watoto ili kuhakikisha wanavikomesha na kujenga watoto walio bora na sio walioharibiwa.

"Hatuwezi kutarajia kupata miujiza ya kuwa na watoto wazuri kwenye jamii wakati sisi wenyewe ndiyo tunaanza kuwajengea ubaya kuanzia kwenye familia, hakuna mtoto ambaye anaweza kuwa bora kwenye jamii wakati ubora huo hakuonyeshwa tangu mwanzo, hatuwezi kukubali hali hii iendelee," alisema Muliro.

Kwa upande wake, Mkuu wa Dawati la Jinsia Kanda hiyo, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Leah Mbunda, alisema ukatili unaongoza kufanyiwa watoto hao ni wa ulawiti, ubakaji pamoja na vipigo.

Alisema miongoni mwa wanaowafanyia watoto vitendo hivyo ni watu waliokaribu nao wakiwamo wazazi, ndugu na wanaoaminiwa au kuwa karibu zaidi na watoto hao.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa WLAC, Theodosia Muhulo, alisema changamoto kubwa iliyo katika kushughulikia mashauri yanayohusu ukatili huo ni kukosa ushirikiano wa ushahidi kutoka kwa wazazi, walezi na wale ambao wanaripoti vitendo hivyo hususani wanapofanya michakato ya kuwafikisha watuhumiwa katika vyombo vya dola.

"Tatizo kubwa linalokwamisha mapambano dhidi ya vitendo hivi ni kukosa ushirikiano kutoka kwa ndugu iwe wazazi, walezi au wale wanaoshuhudia na kutoa taarifa juu ya vitendo hivi, mwanzoni huwa wanatoa ushirikiano mzuri, lakini mnapoanza mchakato wa kufikisha kwenye vyombo vya dola kuanzia kwenda polisi hadi mahakamani, huwa wanakimbia na kwenda kumalizana na watuhumiwa," alisema Muhulo.



Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani wa Benki ya Exim, Colman Riwa (kulia), akipokea tuzo kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali, Leonard Mkude, baada ya benki hiyo kuibuka mshindi wa tatu katika tuzo ya 'Muwasilishaji Bora wa Taarifa za Fedha' kwa mwaka 2020, zilizoandaliwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), mwishoni mwa wiki. Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA, Pius Maneno. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wenye ulemavu wa macho wafaulu masomo

**Na Mary Geofrey**

ASILIMIA 70 ya watoto wenye ulemavu wa macho waliosaidiwa kupatiwa vifaa vya kusomea na kupewa kipaumbele shuleni, walifaulu elimu ya msingi na kijiunga na sekondari.

Hayo yalisema jana na Mkurugenzi wa Shirika la Light For The World, Joseph Banzi, wakati akizungumza na waandishi wa habari, katika mkutano wa wadau mbalimbali wa kujadili namna ya watu wenye ulemavu wanapata fursa ya kuendelea na masomo.

Alisema taasisi hiyo yenye miaka mitano tangu kuanzishwa kwake, iliwasaidia watoto wenye ulemavu kupata elimu na asilimia 30 pekee kati ya idadi yote ndio walioshindwa kuendelea na masomo ya sekondari.

Taasisi hiyo kwa sasa ina jumla ya watoto wenye ulemavu wa macho 311, kutoka katika mikoa ya Mororogo na Dodoma.

Alisema lengo la mkutano huo ni kubadilisha uzoefu kulingana na changamoto za watoto wenye ulemavu na namna kuwasaidia watoto hao.

Alisema yapo mashirika mbalimbali yanayofanya kazi tofauti hivyo wamekutana kuona namna ya kushirikiana katika kuwasaidia watoto hao.

Aidha, alitaja aina ya changamoto zinazowakabili watoto wenye ulemavu ni kukosa matibabu na kukosa vifaa vya kuwasaidia kupata elimu.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), Ernest Kimaya, alisema wanaangalia njia bora zaidi ya kupata elimu jumuishi.

Alisema utafiti unaonyesha kuwa changamoto bado ziko zinazofanya watoto wenye ulemavu kushindwa kupata elimu.

Alizitaja baadhi ya changamoto kuwa ni ukosefu wa walimu wenye taaluma ya ulemavu na vifaa vya kufundishia na kwamba kuna sera za kuwajumuisha wanafunzi wote kupata elimu hata walio na changamoto za ulemavu bila ya ubaguzi.

Pia alisema jamii ina nafasi kubwa ya kuhakikisha inawatambua watoto wenye changamoto ya ulemavu.

"Mara nyingi wanaachwa nyumbani na wengine wanafungiwa ndani. Jamii inaweza kuwasaidia kwa kuwapazia sauti na pia inaweza kuchangia kwenye miundomboni kupitia kamati za shule," alisema Kimaya.

# Makinda kuwatunuku wahitimu 309 Kairuki

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), Spika Mstaafu Anne Makinda, anatarajiwa kuwatunuku wahitimu 309 wa fani mbalimbali wakiwamo madaktari na wauguzi.

Makamu Mkuu wa HKMU, Prof. Charles Mgone, alisema jana kuwa miongoni mwa wahitimu hao ni madaktari 171, wahitimu 84 wa stashahada ya uuguzi, 43 wa shahada ya uuguzi na madaktari bingwa saba wa watoto.

Alitaja wengine wanaotarajiwa kuhitimu mwishoni mwa wiki hii kwenye chuo hicho kuwa ni mhitimu mmoja wa shahada ya umahiri ya ustawi wa jamii na wahitimu watatu wa shahada ya uzamili wa afya ya jamii.

Prof. Mgone alisema kwa mwaka huu wa masomo, chuo hicho kimedahili wanafunzi 237 wa fani ya udaktari, wanafunzi 59 shahada ya uuguzi, tisa wa shahada ya ustawi wa jamii na madaktari bingwa saba afya ya kinamama.

Makamu mkuu huyo alisema wamedahili pia wanafunzi madaktari bingwa 14 wa fani mbalimbali.

Katika hatua nyingine, Prof. Mgone alisema tayari HKMU imeshaanza ujenzi wa kampasi ya Boko ili kukiwezesha chuo kuchukua idadi kubwa ya wanafunzi wa fani mbalimbali.

Alisema HKMU iliamua kujipanua baada ya kuona idadi ya wanafunzi inaongezeka mwaka hadi mwaka na uhitaji wa wananchi kwenye wataalamu wa sekta ya afya unaozidi kuongezeka.

Katika mpango wake wa miaka mitano, alisema HKMU imeanza kuwekeza kwenye matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kukiwezesha chuo kufundisha kwa njia ya mtandao.

"Wakati wa janga la corona tulifundisha kwa njia ya mtandao na sasa tunataka kuimarisha mifumo yetu kuhakikisha tunachanganya, tunafundisha mafunzo ya ana kwa ana na yale ya mtandaoni na tunataka hata shughuli zingine za kiutawala zifanyike online," alisema.




Mshindi wa bodaboda ya Biko, Abbas Mwinyimkuu (katikati), akipokea karatasi za umiliki wa chombo hicho kutoka kwa waendeshaji wa bahati nasibu ya Biko, katika Tamasha la Komaa Concert, lililodhaminiwa na Biko, mkoani Dar es Salaam juzi. Kulia anayekabidhi nyaraka hizo ni Meneja Masoko wa Biko, Goodhope Heaven. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapatiwa mafunzo udhibiti sumukuvu

**Na Mwandishi Wetu,** KILOSA

WAFANYABIASHARA 500 wanaosafirisha na kusindika mahindi, karanga na bidhaa mbalimbali wamepatiwa mafunzo kupitia Mradi wa Kitaifa wa Kudhibiti Sumukuvu (TANIPAC).

Wajasiriamali hao ni kutoka katika wilaya za Kiteto mkoa wa Manyara, Kongwa mkoani Dodoma, Gairo na Kilosa mkoani Morogoro.

Mafunzo hayo yalitolewa hivi karibuni kwa lengo la kudhibiti sumukuvu ili kulinda afya za binadamu, kuwezesha biashara ya mahindi na karanga, kulinda afya za mifugo na kuwezesha utoshelevu wa chakula salama.

Akizungumza wilayani Kilosa wakati wa kufungua mafunzo hayo jana, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania TBS, Jabir Saleh Abdi, alisema serikali kupitia TBS ilianza kutoa mafunzo hayo kupitia Mradi wa Kitaifa wa Kudhibiti Sumukuvu wilayani Kiteto Novemba 24, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Abdi, mradi huo uko chini ya Wizara ya Kilimo na TBS imekabidhiwa jukumu la kutoa mafunzo hayo.

Alisema mafunzo hayo yanatarajiwa kuendelea kutolewa katika wilaya za Kondoa, Chemba, Bahi, Babati, Namtumbo, Newala, Nanyumbu, Nzega, Urambo, Kibondo, Kasulu, Buchosa, Bukombe na Itilima.

Kuhusu mikoa ambayo mafunzo hayo yatatolewa, Abdi alisema ni Dodoma, Manyara, Ruvuma, Mtwara, Tabora, Kigoma, Mwanza, Geita, Simiyu na Morogoro.

Abdi alitaja faida za mafunzo kuwa yamelenga kulinda afya za binadamu, kuwezesha biashara ya mazao ya mahindi na karanga, kulinda afya za mifugo na kuwezesha utoshelevu wa chakula salama.

Alitaja faida zingine kuwa kuhimili ushindani katika masoko ya ndani, kikanda na nje ya nchi na aliwasihi washiriki kuwa mabalozi wazuri wa mafunzo hayo na kuzingatia mambo muhimu yanayoshauriwa na wataalamu ili kudhibiti sumukuvu.

# Taasisi yataka elimu ya uzazi kwa vijana

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi inayojishughulisha na kuwajengea uelewa vijana kuhusu masuala ya uzazi salama (HCCGWT), Halima Lila, amesema kuna umuhimu kwa kuendelea kutoa elimu kwa kundi hilo kuhusiana na namna ya kutambua mabadiliko yao kimwili ili kuwasaidia kufahamu mbinu za kuepukana na maambukizi ya maradhi ikiwamo Virusi vya Ukimwi.

Lila alitoa kauli hiyo wakati akitoa semina kwa vijana mkoani Katavi iliyolenga kuelimisha na kuwajengea uwezo vijana kutoka katika kata 15 mkoani humo namna ya wao kutambua haki zao za msingi katika masuala ya uzazi wa mpango na kuepukana na maambukizi ya maradhi ya Ukimwi pamoja na mimba zisizotarajiwa.

Pia, alisema vijana kuwa na elimu ya kutosha kuhusu masuala ya uzazi wa mpango, kunawasaidia kupunguza na kuepukana mimba za ututoni.

"Pia inawasaidia kuelewa haki nyinginezo ikiwamo namna ya kuchagua mwenza, kuingia katika mahusiano ya kimapenzi ambayo ni salama na haki ya kuchagua wenzi na idadi ya watoto wanaohitaji kwa wakati sahihi," alisema Lila.

Pia alisema ni muhimu kwa vijana wa kike na wanawake, kujitambua kwa kukemea na kukataa kuingia kwenye mtego wa kimapenzi bila kinga pale ambapo inahitajika kufanya hivyo.

"Vijana wa kike na wanawake kuwa na uelewa wa kutosha na kujitambua kunawasaidia hata kuwa na ujasiri wa kusema hapana kuingia katika mtego wa kimapenzi ambao ni hatari kwao hajalishi wako katika mazingira gani na hii ndio elimu ambayo tunasisitiza waipate kwa sababu pia inasaidia kupunguza mimba zisizotarajiwa na hata kuepukana na magonjwa," alisema Lila.

Ofisa Afya ya Uzazi na Watoto wa Wilaya ya Mpanda, Muna Mpanda, alisema ni vema vijana wakatambua kwamba mahusiano salama ni yale ambayo yanalenga kuwalinda wapenzi wote wawili wa kike na wa kiume.

Aliwashauri kwamba kwa kijana anayemthamini na kumlinda mpenzi wake ni lazima atumie kila mbinu za kumlinda anapoona kuna dalili ya hatari iwe kwenye maambukizi ya maradhi au mimba zisizo tarajiwa kwa kutumia kinga ikiwamo kondomu.

# Nipashe yasaidia daraja kukarabatiwa Iringa

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imeanza ku-karabati daraja katika Kijiji cha Mgowelo, Kata ya Nyanzwa, wilayani Kilolo mkoani Iringa, baada ya miezi minne iliyopita kuripotiwa kukwamisha usafirishaji wa abiria na mizigo kutokana na ubovu.

Daraja hilo ni kiunganishi kati ya vijiji vya Nyanzwa, Mgowelo na Mtandika na linategemewa na wakazi wa vijiji hivyo kusafirishia mizigo na shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Akizungumza kwa njia ya simu na mwandishi wa gazeti hili, Diwani wa Kata ya Nyanzwa, Bonifas Mgwale, alisema tangu taarifa za daraja hilo ziripotiwe na gazeti la Nipashe kumejitokeza watu mbalimbali kutoka wilayani kukagua na sasa ujenzi umeanza.

"Tunalishukuru gazeti la Nipashe kwa kututolea habari ya ubovu wa daraja letu na kilio kikafika mbali hatimaye leo daraja la kiwango cha juu limeanza kujengwa," alisema.

"Pia Nipashe limekuwa miongoni mwa chombo cha habari cha msaada kwetu hata kipindi tulipokuwa tunazongwa na tembo kwenye kuharibu mazao ilitoa habari na tatizo likashughulikiwa."

Mbunge jimbo hilo, Lazaro Nyamoga, alipotembelea daraja hilo alibainisha kuridhishwa na kasi ya ujenzi huku akiwataka wasimamizi kuongeza spidi kukamilisha kazi hiyo mapema.

"Leo nimefika hapa kujionea ujenzi wa daraja hili la Kijiji cha Mgowelo, lakini niwaombe mainjinia mnaosimamia daraja hili mfanye kazi kwa spidi ya ajabu kwa sababu msimu wa mvua upo jirani kwa hiyo mkilemaa mvua ikianza itawatesa mtashindwa kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa."

Mwanakijiji Ziaka Geda, alieleza kufurahishwa na kitendo cha serikali kuchukua hatua katika ujenzi huo wa daraja ambalo lilikuwa likikwamisha shughuli za kiuchumi.

"Tangu daraja hilo libomoke mambo mengi yamelala kama kuvusha malishamba kupeleka sokoni."

Mwanahamisi Omari, mkazi wa kijiji hicho aliishukuru Nipashe kutoa habari ambayo imezaa matunda kwa kijiji hicho.

Kamimu Ofisa Mtendaji kijiji hicho, Kumbuka Malenda, aliishukuru serikali kwa kuchukua hatua.



Mtaalamu wa Makazi na Ardhi, Profesa mstaafu Joseph Kironde, akitoa mada kwenye kongamano la kitaaluma lililofanyika kwenye Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU), jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Dk. Tatu Limbumba na Dk. Elinorata Mbuya wote wa chuo hicho. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanasiasa kikwazo shirikisho EAC

**Na Richard Makore,** MWANZA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, amesema wanasiasa wanachangia kukwamisha uundwaji wa shirikisho la kisiasa kwa nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kwa kuhofia kupoteza nafasi walizonazo.

Kwa mujibu wa makubaliano, nchi hizo zinatakiwa kuwa na shirikisho la pamoja la kisiasa ambalo litawezesha pia kuwa na rais mmoja wa kutawala eneo hilo lote.

Aidha, kulikuwa na makubaliano katika nchi hizo kuwa na sarafu moja na soko la pamoja.

Akizungumza katika uzinduzi wa maonyesho ya wajasiriamali wadogo na wakati kutoka nchi sita za Afrika Mashariki, Prof. Mkumbo alisema, wananchi katika nchi hizo hawana shida katika uundwaji wa shirikisho la kisiasa bali wanasiasa ndiyo wamejawa na hofu.

Alisema wananchi wakiwamo wajasiriamali wadogo wao ni wapigakura, lakini wanasiasa ndiyo wanakwamisha kufikiwa na mpango huo kwa kuhofia kupoteza nafasi zao walizonazo.

"Leo hii likiundwa shirikisho hilo, sina hakika kama nitateuliwa kuwa waziri tena, hiyo ndiyo hofu kubwa kwa wanasiasa wengi katika nchi hizo," alisema.

Aliwataka wafanyabiashara hao kutoka nchi za Afrika Mashariki kuboresha shughuli zao na kuwa wabunifu ili kuongeza tija.

Aidha, alisema lengo la serikali ni kuwawezesha wafanyabiashara wadogo na wa kati ili wazalishe bidhaa za kutosheleza mahitaji ya nchi hizo sita.

"Tumeona namba kubwa ya wanawake na vijana wamejitolea kuzalisha bidhaa za ubunifu, serikali itahakikisha inawekeza nguvu katika uwezeshaji wao ili kuhakikisha viwanda vyetu vinapata malighafi ya kutosha inayozalishwa na wazalishaji wadogo na wa kati," alisema Prof. Mkumbo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Shirikisho la wajasiriamali wa EAC, Josephat Rweyemamu, alisema maonyesho hayo yalianza mwaka 1999 yakiwa na washiriki 59 na sasa wameongezeka hadi kufikia 1400.

Aidha, alisema bidhaa zimeongezeka na zingine zimepata nembo za ubora na hivyo kutambulika kimataifa.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, alisema jumla ya wajasiriamali 1,304 wamethibitisha ushiriki na kati ya hao 794 wametoka katika nchi za Kenya, Uganda, Sudan ya Kusini, Burundi, Rwanda na 510 kutoka mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar.

"Maonyesho haya kwetu sisi kwa Wanamwanza ni fursa ya kipekee ya kuandika historia ya mkoa wetu wa Mwanza, yamesaidia kukuza pato la taifa na wajasiriamali pia kupitia mzunguko wa fedha utasaidia mkoa kuongeza mapato," alisema.

Gabriel alisema kuwa Mwanza ni eneo lenye ardhi nzuri na uchumi mzuri na kwamba kuna maeneo mbalimbali ya uwekezaji na ya kibiashara hivyo wafanyabiashara wajitokeze kuwekeza.

Aliongeza kuwa hakuna rushwa wala kuzungushana katika upatikanaji wa maeneo huku akitoa wito kwa wananchi kujitokeze katika maonesho hayo ili kukuza uchumi na kuzitangaza bidhaa mbalimbali za Afrika Mashariki..

Awali Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu( (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu), Jenista Mhagama, alisema tatizo la ajira lipo kwa nchi zote na kwamba maonyesho hayo ni ufunguo wa ajira, kukuza uchumi pia ni nyenzo ya kubadilishana ujuzi ambao unaweza kutengeneza fursa nchini.

Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Maendeleo ya Wajasiriamali Kenya, David Osiany, alisema anafarijika kuona kinamama na vijana wajasiriamali kwenye maonyesho ya mwaka huu ambapo nchini Kenya sekta hiyo inachangia asilimia 83 ya ajira.

Alisema maonyesho ya wajasiriamali yanatoa fursa kuonyesha dunia kuwa wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki si watu wa kununua bidhaa za nje ya nchi zao bali wanao ujuzi wa kutengeneza za kwao wenyewe na kuuziana.

## Wajasiriamali wapewa siri kujijenga kiuchumi

**Na Sabato Kasika**

WAJASIRIAMALI wametakiwa kujipanga kwa ajili ya uchumi wao wa kesho ikiwamo kuwekeza katika jambo ambalo litawasaidia na kuwapa matunda hata wakati uchumi wake utakapokuwa umeyumba.

Hayo yalisemwa na mwezeshaji Emilian Busara, katika kongamano la kuwajengea uwezo wajasiriamali, lililofanyika jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki likishirikisha pia wasomi wa kada mbalimbali.

"Jijengeeni utaratibu wa kuweka mipango endelevu ya maisha yenu kwa miaka kumi ijayo, namna gani mtaishi, uchumi wenu utakuwaje kibiashara ili hata ukiyumba, mtakuwa bado mna akiba ya kutosha," alisema Busara.

Aidha, aliwataka wazazi kufundisha watoto wao wa kike kuanza kujitegemea na kutosheka katika hali zote ikiwa ni pamoja na kuwasikiliza ili kuwajenga kifikra hasa kiuchumi, na kwamba hatakiwi kuwa tegemezi.

Mkurugenzi wa kampuni ya Alaska iliyoratibu mafunzo hayo, Jennifer Bash, alisema, kongmano hilo limepata mafanikio makubwa kutokana na wingi wa washiriki waliojitokeza kupata mafunzo.

## DCB ilivyojipanga kutoa huduma bora

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI Mtendaji wa Benki ya Biashara ya DCB, Godfrey Ndalahwa, amesema wamejipanga kuwekeza katika kutoa huduma bora na zenye viwango vya juu kwa wateja, wanaamini mteja ndio mtaji wao mkubwa katika maendeleo ya benki yao.

Ndalahwa aliyasema hayo Dar es Salaam alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya benki pamoja na ushindi walioupata hivi karibuni kwa kutwaa tuzo ya benki pendwa Tanzania inayotoa huduma bora kwa wateja katika kinyang'anyiro cha mwaka huu cha Tuzo za Chaguo la Mtumiaji Afrika (CCAA).

Alisema ushindi wa DCB katika kipengele cha benki inayotoa huduma bora kwa wateja ni faraja kubwa sana kwa benki hiyo kwani ushindi wa tuzo hizo unapatikana kwa kupigiwa kura na wateja, hii imeonyesha imani kubwa walionayo wateja wao.

"Hii ni mara ya kwanza DCB kushiriki katika kinyang'anyiro kile, Tanzania ina idadi ya benki nyingi tu, kwa benki yetu kupata ushindi huu si kitu kidogo kwetu, ni imani yetu wateja wetu na watanzania kwa ujumla wataendelea kutuunga mkono ili tuweze kufanya vizuri zaidi," alisema Ndalahwa.

HABARI KITAIFA

# Maeneo hatarishi watoto kufanyiwa ukatili yatajwa

**Na Mary Geofrey**

IMEELEZWA kuwa watoto wapo katika hatari ya kufanyiwa vitendo vya ukatili kwenye mazingira ya nyumbani na shuleni kwa sababu ndio maeneo wanapoishi kwa muda mrefu.

Aidha, unyanyasaji unaoongoza kufanyiwa watoto ni ukatili wa kisaikolojia, kimwili, kingono na kutelekezwa.

Ofisa Ustawi wa Jamii, Mkoa wa Dar es Salaam, Florah Masue, aliyaeleza hayo mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam, katika tathmini ya programu ya kuwalinda watoto kupitia Mradi wa Kuelimisha Umma juu ya Haki za Watoto unaotekelekezwa na Kanisa Katoliki duniani.

Mradio huo nchini unatekelezwa kupitia Redio Maria ya Kanisa Katoliki.

"Utafiti mbalimbali kimataifa nchini kuhusu unyanyasaji wa watoto, unaonyesha kuwa ni wa kwanza na wa aina yake katika Bara la Afrika.

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa, mara nyingi watoto wanakabiliwa na unyanyasaji na matukio mengi yanayojumuisha ukatili," alisema Masue.

Alieleza kuwa, serikali imeamua kushughulikia matukio hayo kwa kuridhia mikataba ya kutokomeza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake mwaka 1985 ambao umekuwa chombo cha kupambana na matukio ya ubaguzi.

Naye Mratibu wa Mradi huo, Antipacy Shinyambala, alisema wazo la kuanzisha vipindi vya haki za watoto, limetokana na mkutano ulioitishwa na Papa Francis Februari mwaka 2019 huko Vatican.

Katika mkutano huo, maaskofu wote Wakatoliki duniani kupitia mabaraza ya nchi zao, kuandaa mpango kabambe wa mafundisho ya haki za watoto ili kumlinda mtoto dhidi ya vitendo vya ukatili kuanzia anapotungwa mimba, kuzaliwa na makuzi yake.

Alitaja malengo mengine ya mradi ni kuelimisha umma juu ya haki na nafasi ya mtoto katika jamii. Hii inafanyika kwa kuandaa programu elimishi juu ya umuhimu wa kuwalinda watoto.

Jambo lingine ni kuwachagiza wazazi kuwa wadadisi kwa mabadiliko yoyote wanayoyahisi kwa watoto wao na kubaini madhara ya mabadiliko hayo na watoto wanavyopaswa kufanya wanapopatwa na madhila hayo.

Alisema pia kupaisha sauti za vilio vya watoto visikike kwa sauti ya juu, kwa utulivu na kwa umbali mrefu.



Mhasibu Mkuu wa Serikali, Leonard Mkude (kushoto), akimkabidhi Mkurugenzi wa Fedha wa Vodacom Tanzania Plc, Hilda Bujiku, tuzo ya mshindi wa kwanza kwa uandaaji bora wa taarifa za fedha kwa mwaka 2020 kwa taasisi, makampuni pamoja na mashirika zinazotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shirika Marekani lafadhili wanafunzi masomo

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Marekani PEPFAR kupitia Asasi ya Datalab ya Tanzania limetoa ufadhili kwa wanafunzi wanne wa Tanzania kusomea Shahada ya Uzamili katika takwimu (data).

Wanafunzi hao wameanza masomo yao mwaka huu katika Chuo cha Mawasiliano na Teknolojia (CoICT) cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Walionufaika na ufadhili hao ni Saimon Machera, Nurat Karamagi, Rachel Butoto na Mwantumu Mbaga ambao tayari walikuwa na Shahada ya kwanza waliyoipata chuoni hapo kuhusu masuala ya TEHAMA.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Masauni, aliwakabidhi wanafunzi hao vyeti vya ufadhili huo jana kwenye ufunguzi wa tamasha la kitakwimu (Data Tamasha 2021), huku akiwataka kusoma kwa bidii kwani nafasi walizopata zimekuwa zikitafutwa na watu wengi.

Alisema wanafunzi hao wamebahatika kupata ufadhili huo hivyo wanatakiwa kuwa na bidii katika masomo yao ili kuwavutia waliowafadhili ili waweze kusaidia wenzao kupata ufadhili kama huo.

Alisema akiwa na wajibu wa kusimamia sekta ya fedha na mipango angependa kuona asasi ya Datalab pamoja na asasi zingine zinafuata miongozo hiyo ipasavyo ili kuondokana na upotoshaji wa kutumia takwimu ambazo zinatoa hali halisi ya nchi.

Alisema katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, matumizi ya huduma za mitandaoni Tanzania yaliongezeka sana ambapo wazalishaji wengi katika sekta zote za kiuchumi walitumia na zimesaidia sana kukuza uchumi wa nchi kwa kipindi chote hadi kufikia wastani wa asilimia 7.0 kwa mwaka.

"Haya ni mafanikio makubwa sana katika kuinua uchumi wa nchi na kwa sasa tunatakiwa kufikiria na kuumiza vichwa vyetu ni kwa namna gani tunaweza kufufua (revamp) uchumi wetu ambao kwa kiasi kikubwa umeathiriwa na janga la ugonjwa wa UVIKO-19," alisema.

"Kumbe matumizi ya takwimu katika vyanzo vipya na vya zamani yatatupatia majawabu ya kutumia mitandao ili itupeleke mbele zaidi kutumikia wananchi wetu kwa ajili ya kuwaletea maendeleo endelevu. Hivyo basi, hatuna budi kujifunza kutokana na uzoefu katika mataifa yaliyoendelea duniani na kuanza utekelezaji wake hapa nchini," alisema.

Alizitaka asasi nyingine za kiraia nchini kuiga mfano mzuri wa asasi ya Datalab kwa ushirikiano walio nao na serikali.

# Mkakati waja kukabili uhaba mafuta ya kula

**Na Dinna Maningo,** TARIME

BAADHI ya wakulima wilayani Tarime mkoani Mara wameanzisha mkakati maalum wa kulima zao la alizeti ili kukabiliana na uhaba wa mafuta ya kupikia.

Wakulima hao kwa sasa wanalima mazao mbalimbali yakiwamo ya mahindi, mtama, mihogo, viazi vitamu, mboga na matunda.

Wakizungumza na Nipashe wilayani Tarime, wakulima hao walisema kuwa wameamua kutenga sehemu ya mashamba yao kulima zao hilo kama njia ya kunusuru ukosefu wa mafuta ya kula.

Mkazi wa kijiji cha Sirari katika Kata ya Sirari wilayani Tarime, Amos Sagara, alisema baada ya mafuta ya kula kukosekana aliamua kutenga shamba ekari 8 kwa ajili ya kulima zao la alizeti.

"Mbali na kazi yangu ya udiwani mimi ni mkulima nimelima shamba la ekari 8 zao la alizeti lengo langu nilitaka kujua kama zao hilo linakubali kwenye ardhi ya Tarime baada ya kuona kuna shida kubwa ya upatikanaji wa mafuta ya kula na bahati nzuri zao hili limestawi sana," alisema.

Mkazi mwingine wa kijiji cha Ng'ereng'ere Kata ya Regicheri Marwa Bhoke, alisema ana shamba la alizeti lenye ukubwa wa ekari 8, na kwamba anapovuna huuza mbegu kwenye kiwanda kinachokamua mafuta.

" Mimi nilikuwa msimamizi wa shamba la Sagara nimeshawishika na mimi kulima baada ya kuona zao hilo limekubali nami nimelilima na limestawi na ninaandaa shamba lingine la ekari 20.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Sylvanus Gwiboha, alisema kuna viwanda vinavyokamua alizeti vipatavyo vinne kati ya hivyo viwili vinafanya kazi na viwili vipo katika hatua ya ukamilishaji ili mwakani 2022 vitaanza kufanya kazi.

"Viwanda viwili vipo Kata ya Susuni na kimoja kipo Mtana ambavyo vimetokana na mapato ya ndani ya halmashauri na kiwanda kingine kimoja ni cha mtu binafsi kipo kata ya Gwitiryo," alisema Gwiboha.

Kwa sasa bei ya mafuta ya alizeti mjini Tarime yanauzwa lita 20 kwa Sh. 90,000 hadi Sh. 93, 000, lita 10 ni Sh. 52,000, lita 5 ni Sh. 25,000 hadi 26,000, lita 3 ni Sh. 16,000 na nusu lita 1.5 Sh. 7,000 hadi Sh. 8,000.




Ukurasa 12

Milima, mabonde ya safari ilikotoka Katiba inayotoa jukwaa la kujifunza



Ukurasa 13

Prof. Kabudi: Utafiti ni muhimu kuandika, kuhifadhi historia ya uhuru



Ukurasa 14

REA, chombo kinachotimiza ndoto ya umeme 1964 na mikakati yake



MIAKA 60 YA UHURU

# Azimio Arusha lilivyotumika kuibua utitiri mipango maendeleo endelevu

- Matunda: Azimio Musoma, Iringa; Ujamaa Vijijini

**Na Peter Orwa**



Shughuli za kilimo katika Kijiji cha Ujamaa zikiendelea. **PICHA: MTANDAO**

KATIKA mfumo wa uongozi wa miaka 24 ya kwanza ya uhuru wa nchi, kuna jambo linaloachwa kama marejeo kuhusu staili iliyoshika mfumo ulioamua mambo makubwa, hata kuwa mwenendo wa mipango na matendo ya nchi.

Ni baada ya kuwapo mfumo wa chama kimoja kitaifa mwaka 1964, chimbuko la uamuzi wa kitaifa muundo wake ukianzia kwenye chama wakati huo TANU na baadaye Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mkutano Mkuu wa chama ulipitisha ama azimio au uamuzi, kisha kuiachia serikali kutekeleza ukiwa ni mwelekeo wa nchi.

Baada ya kuandaliwa Mpango wa Maendeleo ya Nchi (1964 hadi 1969), ni miaka mitatu badaaye TANU ilipitisha Azimio la Arusha, lililotafsiriwa "namna nchi itakavyotawaliwa kwa kutumia siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, ilivyokwishatambulishwa miaka kabla.

Kupitia hilo kulishuhudiwa mabadiliko ya asilimia zote miliki binafsi ikiachwa kuhamia katika kwenye umma kupitia utaifishaji, vivyo hivyo kuma kwa kasi mashirika mapya ya umma na hasa viwanda.

Mpango huo wa maendeleo wa kwanza, mbali na mengine mengi, ulisimama katika falsafa ya mageuzi kutoka "kuzalisha tuzichotumia, huku tukitumia tusichozalisha" hadi "kuzalisha tunachotumia."

### AZIMIO ARUSHA

Zao la mpango huo na Azimio la Arusha la mwaka 1967 ndio mizizi wa kuzalishwa sheria iliyosimamia sheria ya mashirika ya umma -SCOPO iliyodumu kwa zaidi ya mashirika ya umma kabla ya mageuzi makubwa ya kisheria na kisiasa kuanzia miaka 1990, baada ya uhuria wa biashara kuanza mwaka 1985.

Pia, mwaka 1970 kulikuwapo mwongozo mwingine wa TANU ulioibua hoja kuagiza mabaraza ya wafanyakazi katika maeneo ya waajiriwa, hoja iliyodumu kisheria hadi sasa kuwa nyenzo muhimu katika Sheria ya Ajira na Uhusiano wa Kazi inayotumika sasa.

Mwaka 1971, TANU ilitoa mwongozo wake unaohimiza sera ya Ujamaa Vijijini ikilenga kuboresha maisha ya wananchi kwa mujibu wa Azimio la Arusha na siasa ya Ujamaa na Kujitegemea

### AZIMIO LA IRINGA

Katika utekezaji wake ndipo mwaka uliofuata 1972 Azimio la Iringa lililokuwa na kaulimbiu 'Siasa ni Kilimo' lilizaliwa, baada ya Rais Julius Nyerere kwa kofia zote za serikali na chama, alifafanua mahitaji makuu ya maendeleo kwamba vinahitajika vitu vinne; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Siasa ni kilimo iliwataka wananchi vijijini watambue kuwa maendeleo yao yangeletwa na kilimo ambacho kingewawezesha kupatikana chakula cha kutosha na ziada kwa kupatia fedha za matumizi mengine.

Ilieleza changamoto za kilimo na jinsi ya kuzishughulikia kwa kutumia kanuni za kilimo bora. Sera ilitoa majukumu ya usimamiaji chakula na kwamba viongozi wawe mfano wa utekelezaji husika.

Chama kilitakiwa kujadili usimamizi na utekelezaji sera hiyo katika vikao vyake na kuhakikisha utaalamu unatumika kutekeleza 'Siasa ni Kilimo'. Baadaye mwaka 1974 iliboreshwa kwa kupitishwa Sera ya Kilimo cha Umwagiliaji.

### AZIMIO LA MUSOMA

Mwaka 1974 TANU ilipitisha tena Azimio la Musoma lililokuwa na kazi katika elimu kwa wote ikihimiza zaidi elimu ngazi ya msingi, mkakati ulioanza kuchukua sura mara tu baada ya Uhuru wa mwaka 1961, kisha mwaka 1964 ikaingia katika mpango endelevu hadi kukutana na azimio tajwa baada ya muongo mmoja.

Ni azimio lililochukua hatua nyingi kisekta, mfano hai mwaka mmoja kabla kulianzishwa Baraza la Mitihani la Taifa na mwaka mmoja baadaye, ikaanzishwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

Pia Azimio la Musoma liliweka sharti serikali itekeleze kwa vijana wa kiume wanaonuia kuendelea na elimu ya juu, wafanye kazi miaka miwili baada ya kutoka Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), ndipo waliruhusiwa kuendelea masomoni kwa idhini ya mwajiri ikiwa namna kuwanoa kifalsafa kutumikia nchi.

**INAENDELEA UK.12**

MIAKA 60 YA UHURU

# Milima, mabonde ya safari ilikotoka Katiba inayotoa jukwaa la kujifunza

• Simulizi wagombea huru, Sarawat hadi Mtikila




Mchungaji Christopher Mtikila, katika harakati zake za kisiasa, enzi za uhai wake. **PICHA: MTANDAO**

**Na Pasience Mlowe**

NI miaka 60 tangu kupatikana Uhuru kutoka kwa wakoloni wa Kiingereza mwaka 1961. Katika kipindi hicho hadi sasa imepitia vipindi tofauti vilivyoamua siasa na mweleko wa taifa uwe na sura gani.

Ulipopatikana Uhuru wa nchi ya Tanganyika na baadaye Tanzania, ilikuwa na katiba yake ya kwanza. Mwaka mmoja baadaye ikawa Jamhuri, hivyo ikaandikwa Katiba ya Jamhuri ya Mwaka 1962.

Miaka miwili baadaye, Tanganyika ilipoungana na Zanzibar ikapatikana katiba ya tatu iliyojulikana Katiba ya Muungano ya Mwaka 1964.

Itakumbukwa kuwa baada ya Muungano huo taifa liliendelea kuwa na vyama viwili vya siasa yaani Tanganyika African National Union (TANU) na upande wa Zanzibar walikuwa bado wamebaki na Chama cha Afro-Shiraz Party (ASP).

> Mwaka 1965 ikapatikana katiba ya nne iliyojulikana kama Katiba ya Mpito (Interim Constitution).

Hivyo basi, mwaka 1965 ikapatikana katiba ya nne iliyojulikana kama Katiba ya Mpito (Interim Constitution) na miaka 12 na baadaye ikaandikwa katiba ya kudumu ya mwaka 1977, ambayo inatumika mpaka sasa. Ni zao linaloendana na utashi wa karibu kuungana kwa vyama vya ASP na TANU, hata kukazaliwa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Hivyo, Watanzania wanapozungumzia miaka 60 ya Uhuru kisiasa, kimsingi hata vyama vya siasa vilivyopo vimekuwa na mageuzi ya kuleta mabadiliko ndani ya katiba ya nchi.

Maana yake ni kwamba hata leo hii wananchi wanapojadili upatikanaji katiba mpya, ni vyema pia kuanza kuangalia mapana ya mfumo wa vyama na itikadi zake, unavyoweza kuleta mabadiliko makubwa au wataaluma, wanasheria hutamka 'transformation'.

Vyama kwa kawaida hushiriki mara nyingi katika mabadiliko hayo, kuliko nafasi ya wananchi wenyewe kwa ujumla wao, ukiwavua uanachama.

Kumekuwapo uzito siasa inaendelea kubeba kura turufu kushinikiza mabadiliko ya kikatiba, uhalisia hata kushuhudiwa misukumo ya karibuni kuhusiana na madai ya katiba kitaifa na hatua na yaliyojiri kuhusiana nayo.

Ili kuingia kwa wananchi kuwa wabadilishi wa katiba ya watu, kwanza inapaswa kutolewa elimu ya uhakika ya uraia, kisha uandishi wa katiba unaangukia ushirikishwaji umma ambao kwa kiasi kikubwa uwe unajua kile unachofanya, ili kufungua ukurasa mpya katika kujadili maudhui ya katiba hiyo.

**MGOMBEA HURU**

Suala kuwa na mgombea huru si dhana ngeni nchini Tanzania, ndani ya miaka 60 ya Uhuru. Wananchi walishuhudia katika uchaguzi mkuu wa TANU jimboni Karatu, alitokea mgombea huru baada ya chama chake cha TANU kumuengua, alishiriki uchaguzi kama mgombea binafsi na kuibuka mshindi.

Huyo ni Herman Sarwatt, aliyemwangusha mgombea aliyepitishwa na TANU, Amri Dodo. Ni jambo linabaki katika vitabu vya historia.

Kwa mfano huo wa Herman Sarwatt kushinda kwa kishindo dhidi ya pendekezo la chama, inatoa funzo kwamba kiongozi wa watu ni lazima atokane na wananchi wenyewe wa wapigakura.

Mara nyingine inawezekana viongozi bora wa watu wakashindwa kujitokeza na kushiriki uchaguzi kwa sababu ya mifumo ya kitaasisi iliyowekwa na vyama.

Hivyo basi, katika miaka 60 ya Uhuru inayosherehekewa kwa kurejea mfano ya karibuni, mwanasiasa marehemu Christopher Mtikila, alipigania sana haki ya Tanzania kuwa mgombea huru kushiriki uchaguzi katika kipindi cha mfumo wa vyama vingi, uliorejeshwa nchini mwaka 1992, baada ya kufutwa wastani wa miaka 28 kabla.

Hivyo, katika kuenzi harakati hizo na kupanua wigo wa viongozi wanaotokana na watu katika miaka 60 ya uhuru, ipo haja ya kutungwa sheria itakayoruhusu mgombea huru.

***Mwandishi ni mwanasheria kutoka asasi, LawAge Consult & Advocates***

***Maoni: pasience@gmail.com/ pasiencem@lawage.co.tz***

## Azimio Arusha lilivyotumika kuibua utitiri mipango maendeleo

**INATOKA UK.11**

Inatajwa matunda ya uandikishaji wanafunzi katika shule ya msingi yalipanda kutoka wastani asilimia 25 mwaka 1960, hadi asilimia 72 wakati anaondoka madarakani mwaka 1985.

Kwa siasa za nje ya nchi, nako katika mwaka 1974 kukashuhudiwa tena namna msukumo kutoka ndani ya chama- TANU ilipopitisha azimio mwaka huo 1974 kuhusu ukombozi Afrika, hata katika utekelezaji wake, Tanzania ikawa mwenye mkubwa wa nchi zilizopigania uhuru wake.

Nadharia inaweka kumbukukumbu namna azimio hilo lilivyohalalishwa kwa makambi ya wakimbizi kama vile Mpwapwa Dodoma, mkoani Morogoro, Kikwa Tabora na Kigoma, pia Nachingwea kwa watokao Msumbiji, yakawa makazi yao, hadi ahueni ilipokuwa shwari makwao.

**VIJIJI VYA UJAMAA**

Katika mfumo wa uongozi na siasa zilizopita, kunatajwa kulikuwapo vijiji vya kawaida na vijiji vya ujamaa, kulikuwa na shughuli za pamoja.

Utekelezaji wa mfumo wa maisha katika vijiji vya Ujamaa, ulianza mwaka 1967 kutokana na maelekezo ya Azimio la Arusha.

Serikali iliwahamisha watu katika sehemu nyingi na kuwaandalia maeneo mapya panapowekewa huduma nyingi za pamoja kama vile shule na vituo vya afya.

Katika kutafuta msukumo zaidi, mwaka 1974 kuliandaliwa operesheni ya Ujamaa Vijijini ambayo watu hawakutakiwa kuishi mijini bila kazi na wakahamishiwa vijijini, jiji la Dar es Salaam, likaandaliwa vijiji vyake, nje ya mji, ambavyo sasa ni mijini.

Hapo panatajwa maeneo kama vile Kibugumo na Gezaulole (sasa Kigamboni wilayani Temeke) na Tegeta wilayani Kinondoni.

Mwaka 1976 ilipitishwa sera inayohimiza Azimio la Arusha ikitamka kazi ni kipimo cha utu cha kujivunia, ikishanulia uvivu, ulevi na uzururaji ikitaja kuwa 'jambo la aibu' sambamba na dhana ya kujitegemea.

Hata kwa kurejea kitabu kilichoandikwa na Dk. Wilbrod Slaa kuna wakati serikali ilitamka kuchukua uamuzi mzito kuhusu idadi ya watoto nchini, uamuzi uliojadiliwa kwa kina ndani ya chama - CCM, yeye akijumuishwa kushiriki kwa kofia ya uongozi wa kanisa.

Mageuzi ya uamuzi mzito wa mengi ya karibu kuanzia ndani ya baraka ya chama ilipunguza makali baada ya nchi kuingia katika mfumo huria kisiasa na kiuchumi.

Hata inaposhuhudiwa sasa, Katibu Mkuu wa CCM, Godfrey Chongolo, akifanya ziara ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchagzui iliyoko katika maeneo mbalimbali na timu yake na ikiambatana na maagizo, iko wazi ina unasaba na mfumo wa utendaji waliorithi tangu zama hizo, chama kuielekeza na kusimamia serikali yake.

## KABUDI AWAAMBIA WASOMI:

# Utafiti ni muhimu kuandika, kuhifadhi historia ya uhuru

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKATI taifa linaadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika, wataalamu na wasomi wanasema wakati umefika kufanya utafiti wa historia ya uhuru kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Wanasisitiza umuhimu wa utafiti kwa maelezo kuwa uhuru huo ndiyo uliofungua milango ya demokrasia Tanzania na Afrika Mashariki, kwa vile ndilo taifa la kwanza kupata uhuru kutoka kwa Mwingereza.

Harakati za kudai uhuru huo zilihamasisha kupatikana uhuru wa Kenya mwaka 1963, Uganda 1962 na Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964.

Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Palamangamba Kabudi, anasema hayo wakati wa Kongamano la Uhuru wa Tanganyika lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).

Anakumbusha kuwa historia ni muhimu kufahamika kwa kundi kubwa la vijana ambao wasipoifahamu kikamilifu wanaweza kubeza na kudharau juhudi zilizofanyika hadi kupatikana uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.

"Wakati umefika sasa kwa watafiti wetu wakiwamo wa historia kufanya kazi ya kuelezea umuhimu wa Uhuru wa Tanganyika ambao ndiyo ulioleta Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964 kufuatia Zanzibar kufanya mapinduzi na kuung'oa utawala wa kisultani wa Oman na wananchi wazalendo kuwa huru katika nchi yao," anasema.



Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Palamangamba Kabudi. **PICHA: MAKTABA**

Anakumbusha kuwa uhuru umeleta matukio mbalimbali muhimu kama kuzaliwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayounganisha Watanzania wa Bara na Visiwani.

Anaeleza kuwa matunda ya Muungano ni kuwaunganisha wananchi wa pande mbili na kuishi kwa amani na utulivu huku wakifanya shughuli zao za kujiletea maendeleo.

Anaeleza katika kipindi cha miaka 60, Tanzania imekuwa imara katika amani na utulivu huku ikiwa kimbilio kwa raia wa nchi jirani waliokumbwa na misukosuko ya kisiasa, vita vya wenyewe kwa wenyewe na uasi.

"Unapoyataja mafanikio ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika unazungumzia amani na utulivu ambao umekuwa dira ya maendeleo ya nchi na wananchi wake," anasema.

Anaeleza kuwa maendeleo makubwa yamepatikana Tanzania na Zanzibar kutokana na kuwapo uhuru wa Tanganyika hivyo kuna kila sababu ya kulinda ili vizazi vya sasa na vya baadaye vijivunie.

Kabudi anawataka wananchi wa pande mbili hizo kusherehekea Uhuru wa Tanganyika unaotimiza miaka 60 kutokana na mambo mengi yaliyopatikana katika kipindi hicho ikiwa ni pamoja na Tanzania kuwa na utaifa wake na kuheshimika ndani na nje ya nchi.

Anasema jambo jingine la kujivunia ni kuwepo kwa Muungano imara kwa nchi mbili hizo ambao hauyumbishwi na zimeweza kuingia katika uchumi wa kati ndani ya miaka 60 kutokana na kuwepo amani na utulivu katika pande zote za Jamhuri.

Hata hivyo, Kabudi anasema Tanzania ni nchi inayojitahidi kujitegemea yenyewe ya kutumia rasilimali za nchi kama madini, milima na ardhi kujiletea maendeleo hivyo ni jambo la kujivunia.

Anaeleza kuwa uhuru wa Tanganyika umeweza kukifanya Kiswahili kuwa ni lugha ya taifa ambayo pia imetumika kwenye ukombozi inayokubalika na kutumiwa popote ndani na nje ya nchi bila hofu.

Kiswahili ni lugha ya Afrika Mashariki, Muungano wa Afrika (AU) na pia inatumiwa kwenye Ushirikiano wa Maendeleo wa Kusini mwa Afrika (SADC).

"Ukomavu wa kisiasa na umadhubuti wa katiba umeleta maendeleo na kupatikana Rais mwanamke nchini Tanzania na hiyo ni moja faida za uhuru wetu." Anasema Waziri wa Sheria.

Anasema uhuru umeleta maendeleo katika harakati za mageuzi ya maendeleo Tanzania hasa kwenye kuimarisha miundombinu kwenye sekta mbalimbali ikiwamo elimu, afya, kilimo na sekta nyingine muhimu kama ya teknolojia ya mawasiliano.

Akizungumzia kero za Muungano anasema serikali itaweka mbele maslahi ya wananchi na kuzifanyia kazi kero zote zinazohusu Muungano na kukumbusha kuwa zipo ambazo zimeshatatuliwa na zilizobaki zitakwisha ili kupata maendeleo kwa Watanzania wa pande zote mbili za Muungano.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Mohamed Salum, anasema Watanzania wana kila sababu ya kusherehekea miaka 60 ya Uhuru kwa sababu uhuru huo umeleta heshima na maendeleo makubwa kwa wananchi wake.

Anasema viongozi walioshiriki katika kupatikana kwa uhuru Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume, walifanyakazi kubwa hivyo waendelee kukumbukwa na kuenziwa ili vizazi vya baadaye viweze kujua chanzo cha Uhuru wa Tanganyika, Zanzibar pamoja na Muungano.

Anaongeza kuwa Tanganyika na Zanzibar zina maingiliano tangu awali kabla ya Muungano na mapinduzi ya mwaka 1964 walioana, kutembeleana na mahusiano ya kiuchumi.

> "Mbali na hilo, Nyerere pia akaamua kuungana na makundi ya watu maarufu katika jamii, hali kadhalika mijumuiko ya makundi kijamii.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, Profesa Makame Haji, anawataka wananchi hususan vijana kwenda sambamba na viongozi wao katika kulinda na kutetea maendeleo yaliyopatikana baada ya Uhuru wa Tanganyika pamoja na Mapinduzi ya Zanzibar.

Anasema elimu mbalimbali zinatolewa kwa vijana ili kujua historia na mambo yaliyotendeka katika nchi ambayo faida yake ni kubwa katika taifa kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Mkuu wa Chuo anasema kuna kila sababu ya wananchi kuheshimu uhuru huo kutokana na maendeleo yaliyofikiwa ikiwamo kuimarika kwa sekta mbalimbali kama vile elimu hasa ya elimu ya juu, miundombinu na utalii.

Anasisitiza kuwa ni vyema elimu na historia ya Tanzania na Zanzibar zikaendelea kutolewa katika maeneo mbalimbali ili kuvifahamisha vizazi vya sasa vijavyo kujua uhuru na muungano ni nini katika maisha yao ya sasa na jinsi ya kuuenzi na kuudumisha.

Anasema haipendezi wengi kuendelea kuubeza bila ya kujua umuhimu wake katika nchi hizo kwa vile yanayoonekana leo ni matokeo ya kazi Muungano na Uhuru wa Zanzibar na Tanganyika.

MIAKA 60 YA UHURU

JUKWAA LA VIONGOZI

# REA, chombo kinachotimiza ndoto ya umeme 1964 na mikakati yake



Makazi yaliyonufaika na huduma za umeme wa REA vijijini. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sanula Athanas**

Miaka mitatu baada ya Uhuru wa Tanganyika, kulishuhudiwa uamuzi wa aina nyingi unaoshikilia historia ya nchi hadi sasa, kisiasa na kiutendaji serikalini.

Eneo mojawapo linaloendelea kufanyiwa kazi katika mwenendo endelevu ni kuharakisha maendeleo vijijini ambako ndiko Watanzania wengi wanaishi na kuna mifano kadhaa kama katika sekta za elimu, maji na afya.

Mpango wa Maendeleo wa kwanza nchini, 1964 hadi 1969, mwaka 1974, chini ya uongozi wa Rais Julius Nyerere, serikali iliendesha Operesheni Vijiji iliyoanzisha vijiji na vijiji vya ujamaa, lengo ni kufikisha na kuboresha huduma kwa wananchi.

Mwaka 2005 ilichukuliwa uamuzi mzito wa kisheria, kuendeleza fikra na mipango ileile ya 1964 wakazi wa vijijini wapatiwe umeme. Hapo ndipo ikapitishwa Sheria ya Nishati Vijijini ya Mwaka 2005 iliyoanzisha Wakala wa Nishati Vijijini (REA), ingawa utendaji wake ulianza rasmi 2007.

Kuanzishwa wakala huo ni sehemu ya utekelezaji wa iliyokuwa Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2003. Sheria ya Nishati Vijijini pia ndiyo iliyoanzisha Bodi ya Mfuko wa Nishati Vijijini.

Wakala huo ulianzishwa kwa nia ya kuhamasisha, kuratibu na kuwezesha uanzishwaji na uendelezaji miradi ya nishati bora vijijini, ili kuhakikisha kunakuwapo nishati bora vijijini inayochangia katika ukuaji uchumi na kuboresha huduma za jamii.

> Mikakati mingine ni kushirikiana na Asasi za Kiraia na zisizo za Kiserikali (NGO) katika utekelezaji wa miradi ya nishati bora maeneo ya vijijini.

Pia kuna kuboresha maisha ya wananchi wa vijijini katika hali endelevu; na uendelezaji wa miradi ya nishati unaozingatia hifadhi za mazingira na usawa wa kijinsia.

**MAJUKUMU YAKE**

Majukumu ya REA yameainishwa katika Sheria ya Nishati Vijijini; kubuni, kuendeleza na kutoa misaada ya kitaalamu kwa waendelezaji wa miradi ya nishati vijijini; kuainisha na kutathmini miradi ya nishati inayostahili ufadhili wa Mfuko wa Nishati Vijijini; kuwajengea uwezo waendelezaji wa miradi ili kutekeleza mipango endelevu ya nishati vijijini; kuibua.

Pia, inahamasisha na kuwezesha utekelezaji miradi ya nishati vijijini; kuhamasisha matumizi ya nishati bora katika shughuli za uzalishaji mali, kilimo, viwanda vidogo na vya kati na biashara, ili kukuza uchumi vijijini; na kuwezesha upatikanaji matumizi ya nishati bora kwa huduma za ustawi wa jamii vijijini kama vile afya, elimu, maji na mawasiliano.

Sheria ya Nishati Vijijini inaanzisha Bodi ya Nishati Vijijini pamoja na kuainisha majukumu yake, ikiundwa na wajumbe kutoka Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), sekta binafsi, Shirikisho la Benki Tanzania, asasi za kiraia, washirika wa maendeleo na Ushirika wa Watumiaji Huduma za Nishati.

**MKURUGENZI REA**

Mkurugenzi Mkuu wa REA, Hassan Saidy, anasema lengo la kuanzishwa kwa mfuko huo ni kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji na matumizi ya huduma bora za nishati vijijini kwa lengo la kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Mfuko unatoa ruzuku kwa waendelezaji wa miradi ya nishati vijijini kwa niaba ya serikali.

Anasema vyanzo vya mapato ya mfuko huo ni serikalini; tozo ya asilimia tatu kwenye uzalishaji umeme wa biashara; tozo kwenye mafuta; ambayo kwa sasa ni Sh. 100 kwa lita; kwenye mauzo ya mafuta ya petroli na dizeli; Sh. 150 kwa lita ya mafuta ya taa; michango kutoka wakala taasisi za fedha kimataifa na washirika wa maendeleo.

Mkurugenzi huyo anasema, REA imeendelea kuhamasisha na kuwezesha utekelezaji miradi ya nishati vijijini katika maeneo mbalimbali ya mikoa yote nchini.

Anaitaja miradi hiyo inajumuisha kuongeza wigo wa Gridi ya Taifa, miradi ya nje ya Gridi ya Taifa iikwamo mifumo midogo ya kuzalisha na kusambaza umeme katika maeneo ambayo yana vyanzo vya nishati jadidifu.

Mingine ni kufunga mifumo ya umeme jua katika taasisi za serikali na huduma za jamii zilizoko vijijini na mifumo mingine isiyo ya umeme.

Anasema tayari miradi hiyo imewezesha ujenzi wa kilomita 38,296.56 za umeme wa msongo wa kati; kilomita 35,253.43 za umeme msongo mdogo; ufungaji wa transfoma 13,700; uunganishwaji wa wateja 716,847 kwa gharama ya Sh. bilioni 2,661.93.

**MAFANIKIO**

Mkurugenzi anataja mafanikio ya REA ni pamoja na upatikanaji wa umeme Tanzania Bara, mwaka jana ukifikia asilimia 69.6 na anabainisha lengo lao ni asilimia 75 ifikapo mwaka 2025 na asilimia 100 mwaka 2030, ambao ni mwaka wa ukomo wa Maendeleo Endelevu.

Anazitaja taasisi zilizopata umeme vijijini zinajumuisha pampu za maji, taasisi za elimu, afya, biashara na nyumba za ibada ambazo jumla yake ni 39,921.

"Mafanikio mengine yaliyopatikana baada ya usanifu, utekelezaji na usimamizi bora wa miradi ya nishati vijiji ni kutengezea masoko kwa viwanda vya ndani vinavyozalisha vifaa vinavyotumika katika ujenzi wa miradi ya umeme na kufikisha na kusambaza umeme katika makao makuu ya wilaya zote nchini.

"Mengine ni kufunga mifumo ya umeme katika nyumba za wafanyakazi takriban 831 kwenye sekta ya afya na elimu katika mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Kagera, Pwani, Lindi, Mtwara, Ruvuma na Tabora.

"Pia uboreshaji wa kilimo cha umwagiliaji katika mashamba likiwamo shamba la Mtakuja (Kilimanjaro) na Zuzu (Dodoma). Kupunguza uhamaji wa vijana kutoka vijijini kuja mjini kwa kuwa sasa huduma za umeme zinapatikana vijijini, hivyo kuzitumia kwa shughuli za uzalishaji mali.

"Kuanzishwa kwa viwanda vidogo na vya kati; mfano mashine za kusaga, uchomeleaji, saluni za kiume na za kike, viwanda vya useremala; upatikanaji wa burudani vijijini mfano matumizi ya televisheni, redio na disko," anasema.

Mkurugenzi huyo anataja ujenzi wa mitambo ya bayogesi 725 vijijini, kwa ajili ya kuzalisha nishati ya kupikia na kuimarika ujasiriamali, mfano uanzishwaji wa vioski vya vinywaji baridi na uzaji mitandao.

**KAMISHNA UMEME**

Kamishna Msaidizi Maendeleo ya Umeme, Stuyden Rwebangila, anaitaja mikakati ya REA kuendelea kufikisha umeme sehemu ambazo hakujafikiwa, ikihamisha na kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya nishati na umeme vijijini.

Rwebangila anaitaja mikakati mingine ni kushirikisha taasisi za fedha kuwekeza katika miradi ya nishati vijijini na kuhamasisha utekelezaji miradi ya nishati jadidifu kutoka vyanzo vya asili vinavyopatikana katika maeneo ya vijijini na kwenye visiwa.

"Mikakati mingine ni kushirikiana na Asasi za Kiraia na zisizo za Kiserikali (NGO) katika utekelezaji wa miradi ya nishati bora maeneo ya vijijini.

"Kuendeleza upanuzi wa mifumo ya umeme ya Gridi ya Taifa kufikia maeneo mengi zaidi ya vijijini kwa kuwatumia makandarasi binafsi wenye uwezo wa kutekeleza miradi kwa kiwango kinachotakiwa.

"Pia kuibua na kupanga maeneo yatakayopelekewa miradi kutokana na vipaumbele vya taasisi pamoja na taifa kwa kuzingatia mikoa ambayo imefikiwa na huduma ya umeme kwa viwango vidogo," anabainisha.





# Wauguzi, wakunga 1,224 kuapishwa leo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JUMLA ya waauguzi na wakunga 1,224 leo wataapishwa na kupewa vyeti vya usajili na leseni ambavyo watavitumia kwenda kutoa huduma katika maeneo.

Aidha, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, limewaonya waauguzi kuacha kufanya kazi bila kuwa na leseni kwani kufanya hivyo ni kosa kisheria na yeyote atakayebainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Agnes Mtawa, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu majukumu ya baraza hilo kwa mujibu wa sheria.

Alisema wauguzi hao pamoja na wakunga watakula kiapo cha utiifu na kutoa huduma kwa maadili na pia watafundishwa mambo mbalimbali ikiwamo sheria ya uuguzi na kanuni zake, maadili, uwajibikaji na miongozo mingine.

Pia Mtawa alisema ni takwa la kisheria muuguzi kuwa na leseni kwani bila kufanya hivyo atakuwa nafanya kosa.

"Baraza linatoa rai kwa wauguzi wote lazima wawe na leseni na waajiri wahakikishe kuwa wanatoa ajira kwa wauguzi wenye leseni tuu na siyo vinginevyo," alisema Mtawa.

Akizungumzia kuhusu vitendo vya uvunjaji wa maadili vinavyofanywa na wauguzi alisema katika mwaka wa fedha uliopita kulikuwa na kesi nane zilizoripotiwa.

"Vitendo vya uvunjaji wa maadili ya uuguzi vipo kama ilivyo katika kada zingine lakini kwa kipindi cha mwaka wa fedha uliopita jumla ya kesi nane zililipotiwa na kati ya hizo mbili walisimamishwa kutoa huduma za uuguzi mmoja kwa kipindi cha mwaka moja na mwingine miaka miwili waliobaki walipatiwa kalipio,"alisema.

Vilevile, alisema Baraza linawahamasisha wauguzi na wakunga wote nchini kuhakikisha popote watakapokuwa wanajisomea ili kuwa na elimu endelevu ili kuendana na mabadiliko mbalimbali ya teknolojia.

"Hili ni takwa la kisheria ambalo ni lazima lifanyike hili linamwezesha muuguzi na mkunga kuhuwisha leseni yake kila baada ya miaka mitatu. Muuguzi anapokiuka maadili ya kitaaluma kwa mujibu wa sheria ya uuguzi na ukunga anachukuliwa hatua," alisema Mtawa.

Alisema Baraza pia limejikita katika kusimamia maadili ambayo yanaongozwa na misingi saba ikiwemo kuheshimu utu wa mtu na uhai, kuomba ruhusa kabla ya kutoa huduma.

Pia kudumisha weledi wa kitaaluma, wajibu wa uwajibikaji kwa lolote utakalolifanya, kuwa mwaminifu na kuzingatia usawa, kushirikina na watendaji wengine na kulinda siri ya wateja.

# Walimu wapya kupewa mafunzo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Gerald Mweri, amezitaka kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutoa mafunzo kwa walimu wapya ili kuwajengea uwezo kutekeleza majukumu yao kwa weledi.

Aidha, ameziagiza kamati hizo kutoa mafunzo kwa walimu ambao wanaokiuka maadili ya taaluma hiyo na kufanya makosa ya mara kwa mara ili warudi kwenye mstari na kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Akizungumza na Kamati hizo kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Magharibi, Mweri alisema mafunzo hayo yatasaidia makundi hayo kufanya kazi yao kwa kufuata miongozo, sheria na taratibu zilizowekwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya kada hiyo ya ualimu.

"Mafunzo haya mnayoyapata na ninyi mkayatoe kwa walimu wapya huko katika maeneo yenu, lakini wapo walimu ambao walishapewa mafunzo, lakini bado wamekuwa wakifanya makosa ya kujirudia nao nendeni mkawaite na kuwapa mafunzo badala ya kukimbilia kuwapa adhabu,"alisema Mweri. Aidha, alisema kamati hizo zimepewa jukumu la kufuatilia maadili ya walimu huku akisema wanapaswa kuliangalia suala hilo kwa umakini mkubwa na kutoa adhabu inayomstahili mwalimu kulingana na kosa alilolitenda.

"Mkumbuke mmepewa jukumu na mustakabali wa ajira za walimu upo mikononi mwenu, maamuzi mnayoyafanya ni ya kutazamwa na kuyafanya kwa kutenda haki, kwenye kosa mwalimu apewe adhabu anayostahili lakini, msisubiri watu wafanye makosa ili wawaadhibu.

"Muwajengee walimu wapya uwezo, pia na walimu ambao hawaendi sawasawa muwape mafunzo, maana serikali haipendi mwalimu afukuzwe kazi maana unakuta wengine tayari wana uzoefu wa miaka kumi, kwa hiyo tunapenda wabaki shuleni,"alisema Mweri.

Mweri, alizitaka kamati hizo kuhakikisha chombo hicho kinakuwa baraka katika kutatua na kupunguza changamoto za walimu badala ya chombo hicho kugeuka laana.

Alisema, kwa upande wa TAMISEMI itaendelea kushirikiana na TSC katika kuhakikisha mnapata vitendea kazi.

Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba, alisema mafunzo hayo yatawawezesha watendaji hao kusimamia sharia, kanuni na taratibu kama zilivyowekwa katika ajira zao.

"Tume hii imeamua kuendelea kuwapatia watendaji mafunzo ili wajitambue wao ni wakina nani na si kuwaacha wafanye makosa ndipo waadhibiwe au kufukuzwa kazi, ukishamfukuza mwalimu kutafuta pengo lingine la kuziba ni kazi, hivyo tutaendelea kutoa mafunzo haya kwa awamu kutokana na upatikanaji wa fedha," alisema Prof. Komba.

Aidha, alisema tangu waanze kuwawezesha watendaji hao wa kamati za wilaya malalamiko yamepungua kwa kiasi kikubwa na tayari wameshazifikia kanda tano kwa ajili ya utoaji mafunzo hayo.

Awali, Katibu wa TSC, Paulina Nkwama, aliwataka wajumbe wa kamati hizo za wilaya kuwa wasikivu kwa kuwa watajifunza mafunzo ambayo yatasaidia kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.



Mjasiriamali Penina Kaminyonge mkazi wa Makole, akiandaa bidhaa zake katika maonyesho ya Wiki ya Wajasiriamali, viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma jana, ikiwa sehemu ya madhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri aagiza msako silaha zisizosajiliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, ameliagiza Jeshi la Polisi kufanya msako kwa kutumia taarifa za kiintelijensia ili kuwabaini na kuwakamata wanaomiliki silaha kinyume na sheria.

Simbachawene alibainisha hayo ijini Dodoma alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa tangazo la serikali la msamaha wa usalimishaji silaha haramu kwa hiari.

"Mtakumbuka kwamba Oktoba 30, 2021 nilitangaza msamaha wa kutoshtakiwa kwa yeyote atakayesalimisha silaha kwa hiari kuanzia Novemba 1-30, mwaka huu.

"Hii ilitokana na tangazo la serikali Na. 774 la tarehe 29/10/2021 ambalo liliainisha masharti ya usalimishaji wa silaha kwa hiari," alifafanua Simbachawene.

Alisema hatua hiyo ya kutangaza msamaha wa usalimishaji wa silaha zinazomilikiwa kinyume na sheria ilitokana na kifungu cha 64 cha sheria ya usimamizi na udhibiti wa silaha na risasi ya mwaka 2015.

"Masharti yaliyoainishwa katika Tangazo la Serikali kuhusu msamaha wa usalimishaji wa silaha haramu kwa hiari yalikuwa kama ifuatavyo usalimishaji wa silaha ufanyike kuanzia tarehe 1/11/2021 hadi 30/11/2021 silaha hizo zisalimishwe kwenye kituo chochote cha Jeshi la Polisi.

"Ofisi za serikali za mitaa, ofisi za watendaji wa kata muda wa kusalimisha silaha ni kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa 10:00 jioni," alisema.

Kadhalika, alisema katika kuratibu zoezi hilo, Jeshi la Polisi liliendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kusalimisha silaha za moto zinazomilikiwa kinyume cha sheria kupitia vyombo vya habari vikiwamo redio, televisheni na mikutano ya hadhara. Hata hivyo, alisema matokeo ya usalimishaji wa silaha hadi kufikia Novemba 30, 2021 zilizosalimishwa ni 228.

"Pistol tano sawa na asilimia 2.2 ya silaha zote zilizosalimishwa, magobore 174 sawa na asilimia 76 ya silaha zote zilizosalimishwa, Shortgun 38 sawa na asilimia 16.7 ya silaha zote zilizosalimishwa, Rifle 10 sawa na asilimia 4.4 ya silaha zilizosalimishwa na SMG moja sawa na asilimia 0.4 ya silaha zote zilizosalimishwa," alisema.

Pia alisema imesalimishwa jumla ya mitutu 12 ambapo mitutu 11 imesalimishwa Mkoa wa Tanga na mtutu mmoja umesalimishwa Mkoa wa Mbeya.

Alisema kati ya silaha zilizosalimishwa imeonekana kuwa magobore ni asilimia 76.3, jambo linaloonyesha kuwa tatizo la utengenezaji wa silaha za kienyeji yakiwamo magobore ni kubwa nchini.





# Ukosefu wa virutubisho udongo chanzo kupungua tija uzalishaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UDONGO wa mashamba mengi ya wakulima nchini hauna virutubisho muhimu kwa ajili ya ustawi wa mazao na baadhi ya mashamba yana tindikali ambayo inapunguza tija kwenye uzalishaji wa mazao.

Utafiti maalum wa afya ya udongo ambao umefanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Uyole kwa kushirikiana na Kampuni ya Usambazaji wa Mbolea ya OCP, umebaini hali hiyo na kupendekeza hatua za kitaalamu zichukuliwe haraka ili kuongeza tija kwenye kilimo.

Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, aliyasema hayo wakati wa kukabidhi ripoti ya utafiti huo kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya. Alisema utafiti huo ulifanyika katika mikoa ya Rukwa, Mbeya, Iringa na Morogoro.

Alisema katika kila mkoa, walipima afya ya udongo kwenye vijiji 100, kila kijiji mashamba 30 na kuwafundisha wakulima namna na kukabiliana na matatizo yaliyomo kwenye udongo wa mashamba yao.

Dk. Bucheyaki alisema katika mikoa hiyo walibaini kuna upungufu wa madini mbalimbali yakiwamo ya phosphorus, boron, zinki na salfa ambayo ni muhimu kwa ukuaji wa mazao na kwamba kwa mkoa wa Iringa mashamba mengi yana tindikali.

"Katika kila eneo tumewashauri wakulima aina ya mbolea wanayostahili kuitumia kwenye mazao yao na kiasi cha kutumia. Pia kwenye kila kijiji tumewafundisha maofisa kilimo 30 kwa ajili ya kusaidia kuwafundisha wakulima na tumewafundisha wakulima 10,000 kwenye kila mkoa," alisema Dk. Bucheyeki.

Mkurugenzi wa Kampuni ya OCP Tanzania, Dk. Mshindo Msolla, alisema kampuni hiyo iliamua kushirikiana na TARI kufanya utafiti ili kuwasaidia wakulima kutambua afya ya udongo wa mashamba yao na wawe na chaguo sahihi la mbolea za kutumia.

Alisema lengo kuu ni kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao ili kuliwezesha taifa kuwa na uhakika wa chakula pamoja na kuuza ziada nje ya nchi na kuongeza kipato kwa wakulima na taifa.

Dk. Msolla alisema awali walishirikiana na TARI kufanya utafiti ili kubaini mbolea zinazosambazwa na kampuni hiyo kwa wakulima kama zina ufanisi unaostahili hasa kwenye kilimo cha mahindi na mpunga.

Alisema kwa sasa wamepata maombi mengine kutoka serikalini kwa ajili ya kufanya utafiti wa namna ya kuongeza tija kwenye uzalishaji wa korosho na kwamba watashirikiana na TARI Kituo cha Naliendele, Mtwara.

"Lakini tumeombwa tushirikiane na serikali kufanya utafiti kwa ajili ya kuongeza tija kwenye uzalishaji wa michikichi. Tunashukuru Waziri Mkuu anatupatia ushirikiano mkubwa na tutafanya hivyo maana serikali inatumia zaidi ya Dola milioni 400 kuagiza mafuta nje ya nchi," alisema Dk. Msolla.

Akipokea taarifa ya utafiti huo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka wakuu wa wilaya za mkoa huo kuitumia ripoti hiyo kuwahamasisha wakulima aina ya mazao wanayostahili kuzalisha kulingana na afya ya udongo wao.

Homera aliziomba taasisi hizo kuendelea kufanya tafiti za aina hiyo ili kuwasaidia wakulima kuongeza tija kwenye uzalishaji huku akiahidi ofisi yake kuwapatia ushirikiano kwenye kazi hiyo.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Usambazaji wa Mbolea ya OCP Tanzania, Dk. Mshindo Msolla (kushoto), akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, taarifa ya utafiti wa afya ya udongo katika mkoa huo jana, uliofanywa kwa ushirikiano kati ya kampuni hiyo na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole. Kulia ni Katibu Tawala wa Mkoa huo, Dk. Angelina Lutambi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## T-MARC yageukia maambukizi ya VVU

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la T-MARC Tanzania limesema litaendelea kushirikiana na serikali kupambana na maambukizi ya virusi vya Ukimwi kwa kuhamasisha wananchi hasa vijana kutumia kondomu ili kujikinga.

Pia shirika hilo linalosambaza kondomu nchini, limeipongeza serikali kwa jitihada mbalimbali ambazo inazichukua ili kuhakikisha inafikia malengo ya dunia ya kumaliza maambukizi ya VVU ifikapo mwaka 2030.

Mwakilishi wa T-MARC Tanzania, Oliveria Tarimo, aliyasema hayo juzi alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari mkoani Mbeya kwa lengo la kutoa tathmini ya ushiriki wa shirika hilo kwenye maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani ambayo kitaifa yalifanyika jijini Mbeya.

Alisema kwenye maadhimisho hayo, shirika lilijikita kwenye utoaji wa mafunzo ya matumizi sahihi ya kondomu za Dume Classic, Dume Desire na Dume Extreme ambazo alisema zinawafaa watu wa rika mbalimbali na kipato tofauti.

Tarimo alisema msisitizo zaidi wa elimu hiyo ulikuwa kwa vijana na watu walio kwenye maeneo hatarishi huku akidai kuwa waliwalenga vijana kwa sababu takwimu za maambukizi mapya zinaonyesha ndilo kundi linaloathirika zaidi.

"Sisi kama shirika ni washirika wa karibu wa serikali ya Tanzania katika vita dhidi ya Ukimwi. Kupitia maonyesho ya safari hii tulipata nafasi ya kuihudumia jamii kama sehemu ya mchango wetu na vijana wakiwa kwenye kundi tunalolilenga zaidi," alisema Tarimo.

Alisema maonyesho ya mwaka huu yalikuwa rafiki na yenye kuwezesha taasisi zilizoshiriki kupata nafasi ya kufanya kile walicholenga ikiwemo kutoa elimu kwa wadau mbalimbali waliotembelea mabanda na kupata ushauri.

Kuhusu hali ya utoaji wa huduma kwa jamii kwenye mapambano dhidi ya maambukizi mapya ya VVU alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita shirika hilo lilisambaza nchini kondomu milioni 60.

# Mjadala waliokatisha masomo wapamba moto

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAZAZI na walezi wilayani Chunya. wameliomba Bunge kutunga sheria ya kusimamia uamuzi wa kuwarejesha shuleni watoto wa kike waliokatisha masomo kwa sababu ya ujauzito ili kudhibiti ongezeko la mimba na nidhamu ya watoto.

Ombi hilo lilitolewa juzi na wazazi katika mahafali ya shule ya awali na msingi ya Kengold huku wakisema licha ya serikali kuwa na nia njema ya kuwasaidia watoto wa kike, suala hilo lisipotungiwa sheria linaweza kuwa na madhara makubwa.

Mmoja wa wazazi hao, Alfred Kaminyoge, alisema waliupokea kwa hofu uamuzi wa serikali wa kuwarejesha shuleni wanafunzi waliokatisha masomo kwa kupata mimba kwa vile wanaamini uamuzi huo unaweza kuchochea vitendo vya watoto kupata mimba katika umri mdogo.

"Uamuzi wa serikali ukiutazama kwa haraka haraka utaona kuwa ni wenye nia njema ya kuwasaidia watoto wa kike kupata elimu. Lakini kiukweli kama hakuna utaratibu maalum wa kusimamia suala hili, inawezekana ukaharibu watoto wengi zaidi," alisema Kaminyoge.

Alisema kutokana na hali hiyo, wanaliomba bunge kutunga sheria ya kusimamia eneo hilo ili kuweka utaratibu wa namna ya wasichana waliokatisha masomo kwa kupata mimba kurejea masomoni.

"Kama hakutakuwa na sheria mahsusi, kuna hatari ya wasichana wengi kuacha masomo na kuendekeza vitendo vya ngono wakijua hata wakipata mimba watarejeshwa. Pia kuna uwezekano wa msichana mmoja kupata mimba zaidi ya mbili kabla ya kumaliza masomo jambo ambalo pia si zuri, hivyo uwepo wa sheria ni muhimu," alisema Kaminyonge.

Naye Hekta Siame alisema kuwa sheria inahitajika kusimamia suala hilo ili kudhibiti hata wanaume wanaowapa mimba wanafunzi ili kuwalinda watoto wa kike na mimba za utotoni.

Alisema endapo hakutakuwa na sheria, wanaume wenye tabia ya kufanya mapenzi na wanafunzi wataendelea wakijua kuwa hata wakipata mimba watarejeshwa shuleni.

"Kutokana na uamuzi huu wa serikali, hakuna yeyote atakayekuwa na hofu ya kumpa mimba mwanafunzi. Vitendo hivyo vitaongezeka, maadili yatashuka na hata maendeleo ya elimu yataporomoka. Ni lazima itungwe sheria ambayo itasimamia suala hili na kuwalinda watoto wetu," alisema Siame.

Mmiliki wa Shule ya Kengold, Kenneth Mwambungu, alisema kwa kawaida mwanafunzi akipata mimba akajifungua na kurejeshwa tena shuleni, kunakuwa na uwezekano mkubwa wa kuporomoka kitaaluma.

Aliwaomba wazazi kwamba pamoja na uamuzi huo wa serikali, lakini kila mmoja anatakiwa kuhakikisha anashiriki kuwalinda watoto hao dhidi ya mafataki ili kuepusha ongezeko la mimba shuleni.





# Mrajis: Maboresho yanahitajika mahakamani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MRAJIS wa Mahakama Kuu Zanzibar, Muhamed Ali Muhamed, amesema Mahakama inahitaji maboresho makubwa hasa katika uendeshaji wa kesi kutokana na kulalamikiwa katika utendaji wake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa baada ya mkutano wa majaji, mahakimu na wakuu wa Chuo cha Mafunzo (Magereza) ulioandaliwa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), alisema malalamiko hayo yamejikita zaidi katika uendeshaji wa kesi, ucheweleshaji wa hukumu, ucheweleshaji wa uendeshaji wa kusikiliza mashahidi na rushwa.

Mrajis huyo alisema mfumo wa mahakama ni mchanga, hivyo unahitaji kuendelezwa ili mahakama ionekane kikanda, kitaifa na kimataifa.

Alisema kuna wimbi kubwa la kesi za udhalilishaji na kwamba kwa mwaka huu, Mahakama ya Mkoa Vua ilipokea kesi 543 wakati Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja ilipokea 55 na ile ya Mkoa wa Kusini Unguja kesi 62.

Licha ya kuongezwa mahakimu 13 wa mkoa kwa ajili ya kusikiliza kesi za udhalilishaji, alisema bado kasi ya usikilizaji wa kesi ni mdogo kwa sababu matukio ni mengi na mahakimu ni wachache.

"Azma ya Kaimu Jaji Mkuu wa Zanzibar ni kuhakikisha walipangiwa kesi za udhalilishaji yaani, mahakimu maalum kusikiliza kesi hizo pekee, zinasikilizwa kwa haraka na kutolewa uamuzi.

Pia alisema bado hali si shwari Zanzibar kuhusu matukio ya udhalilishaji na dawa za kulevya, hivyo elimu inatakiwa kutolewa kwa jamii ili kuzuia mambo hayo katika jamii.

"Hali ya gereza si nzuri kwa kuwa mrundikano wa watu ni mkubwa kutokana na matukio hayo kuongezeka na kesi hizo hazina dhamana. Kwa siku gereza hupokea wastani wa watu saba," alibainisha.

Mrajis alikiri kuwa kuna kesi nyingi za kusingiziwa baada ya kuwa kesi za udhalilishaji kutokuwa na dhamana, hivyo baadhi ya familia hulipizana visasi kwa kusingiziana ndiyo maana baadhi ya kesi zinakosa ushahidi.

Naye Mkuu wa Sheria Chuo cha Mafunzo, Mrakibu Mwandamizi Seif Maabadi Makungu, alisema hatua mbalimbali zinachukuliwa ili dhana ya haki za binadamu kutekelezwa kwa vitendo na kuna baadhi ya majengo ya magereza yanaruhusu kupata huduma za kibinadamu wafungwa wakiwa katika vyumba vyao.

Alisema wafungwa wanapata fursa ya kufanya ibada na hupatiwa elimu angalau kujua kusoma na kuandika kwa wale ambao hawajapata elimu ya lazima.



Mkuu wa Mkoa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, akizungumza na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), mkoani humo jana. **PICHA: TRA**

# Bidhaa za ndani zapigiwa debe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATANZANIA wametakiwa kujenga utamaduni wa kuthamini bidhaa zinazozalishwa nchini ili kuwapa nguvu wawekezaji wa ndani katika kuzalisha na kuinua sekta ya viwanda.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdull, alisema hayo jana wakati wa ufunguzi wa maonyesho ya sita ya bidhaa za viwanda uliofanyika katika viwanja vya Maisara, mjini hapa.

Alisema Tanzania ina kila aina ya bidhaa zenye sifa na ubora, hivyo katika kuunga mkono jitihada za wazalishaji, hakuna budi kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini.

Hemed aliwataka washiriki wa maonyesho hayo kushiriki katika matukio mbalimbali ikiwamo mikutano ya kibiashara na kongamano la viwanda. Alisema kufanya hivyo kutawasaidia kujifunza, kubadilishana uzoefu na kukutana na wanunuzi wa bidhaa wanazozalisha.

Alisema Serikali ya Muungano na ya Zanzibar ziko katika mchakato wa kuimarisha mazingira mazuri ya viwanda kwa lengo la kuhimili ushindani wa masoko kwa kuwa na bidhaa bora zenye viwango.

Katika kuhakikisha lengo hilo linafanikiwa, alisema serikali ya Zanzibar imetenga Sh. bilioni 84.5 kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali kuimarisha biashara zao.

"Na kwa vile serikali imejikita katika kuendeleza uchumi wa buluu, kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 36.5 zitaelekezwa katika sekta ya uvuvi na mazao ya baharini hususani mwani na dagaa," alisema.

Hemed alisema serikali inaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa kiwanda cha mwani Pemba ambacho kitasaidia kuongeza thamani ya zao hilo na pato la wananchi.

Naye Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban, alisema tangu kuasisiwa kwa maonyesho hayo mwaka 2016, wenye viwanda 500 wameshiriki na kwa mwaka huu wameshiriki 113 vikiwamo viwanda 10 vya Zanzibar na 23 kutoka Tanzania Bara.

Kauli mbiu ya maonyesho hayo ni "Tumia Bidhaa za Tanzania, Jenga Tanzania".

## Kaya 1,050 kunufaika na mazao viungo biashara

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

KAYA 1,050 nchini zinatarajiwa kufaidika na mradi wa kilimo hai cha mazao ya biashara ya viungo kupitia mradi wa Agri-Connect unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU).

Akizungumza jana wakati wa ufunguzi wa Kongamano la kilimo hicho Chakechake, kisiwani Pemba, Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, Soud Nahoda Hassan, alisema ushirikiano wa taasisi za kilimo hicho kwa Zanzibar na Tanzania Bara utakuza maendeleo ya Tanzania.

Soud alisema Zanzibar lazima iendane na mchakato wa kuendeleza kilimo hai ili kutoa tija kwa wazalishaji na kuleta ustawi kwa wananchi na serikali kwa ujumla.

Alisema kilimo hai ni moja ya mambo ambayo yatasaidia kuingia katika sekta ya utalii kwa vile itakuza uingiaji wa wageni kufika nchini kuangalia na kununua bidhaa hiyo baada ya kujionea uzalishaji wa viungo hivyo.

Waziri Soud alisema Tanzania ina aina 30 ya viungo hao vikiwamo karafuu, pilipili manga, tangawizi, vanila, pilipili kichaa, mdalasini, iliki na mchaichai ambavyo vinatumika kwa chakula na dawa.

"Kihistoria uzalishaji wa viungo kwa Tanzania uko vizuri hasa vile vinavyotoka Pemba, hivyo naomba ushirikiano baina ya taasisi hizi uendelee kwa kuleta faida kwa wazalishaji na serikali kwa ujumla," alisema Soud.

Alisema mwaka 2015 Zanzibar ilikuwa ikizalisha tani 8,609 na tani 396 (asilimia 4.29) ilitumika kwa usafirishaii , lakini mwaka 2019 usafirishaji uliporomoka licha ya kuongezeka kwa uzalishaji kwa tani 38,987 kwa mwaka.

Waziri alisema karafuu ni zao pekee ambalo lilikuwa likichukua zaidi ya asilimia 90 katika kusafirisha kwenye soko la viungo duniani ingawa Tanzania ina mpango wa kuongeza usafirishaji wa viungo katika miaka 10 hadi 15 ijayo.

Akitoa maelezo ya mradi huo kwa wafadhili kutoka EU, Colin Scott alisema mpango huo unaofadhiliwa na jumuiya hiyo utaboresha maisha ya wakulima wadogo katika Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania na Zanzibar.

Alisema kuwa utachangia ukuaji wa uchumi, maendeleo na uwekezaji katika sekta binafsi, utengenezaji wa ajira na kuboreshwa kwa usalama wa chakula na lishe.

Hata hivyo, alisema utasaidia uboreshaji wa sera zinazojenga mazingira wezeshi na uwekezaji zaidi wa sekta binafsi, kuendeleza minyororo ya thamani kwa kuboresha uzalishaji, usindikaji na uuzaji.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ANATAFUTWA



**PASCHAL MASHAKA SHIJA**

Mwenye picha hapo juu anatafutwa kwa tuhuma za wizi wa fedha na mali. Jalada la ripoti **KMR/RB/9185/2021.** Yeyote atakayemuona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0718 933 780 / 0685 990 087.**

116604002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

**OMBI LA URAIA WA TANZANIA**
**HII NI TAARIFA KUWA:**



**SYLVIE MARIE ANGE NIYITEGEKA**
**S.L.P 5111, DAR ES SALAAM.**

Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mhe. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni RWANDA. Nchi atokayo ni RWANDA. Shughuli zake ni MAMA WA NYUMBANI na anwani yake ni S.L.P 5111, Dar es salaam. Yupo hapa nchini tangu 2010. Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa kwa maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji S.L.P 512, Dar es salaam. Kumb Na. DN. 137609.

Kny: KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI

116605602

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**(IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA)**
**AT ARUSHA**

**MISC. LAND APPLICATION NO 58 OF 2020**

**(C/f The High Court of Tanzania Land Apeal No 20 of 2017 and Original Karatu District land Housing Tribinal application No 22 of 2008)**

**JOSEPH LOHAY AKONAAY……………………………..APPLICANT**

**VERSUS**

**PASKALI CLETI MAGWAY……………………………….. RESPONDENT**

**NOTICE OF MENTION**

**TO: PASKALI CLETI MAGWAY.**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the High court at Arusha on 14th day of DECEMBER,2021 AT 09:00am in the forenoon. You may appear in person

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time for mention, the court may proceed in your absence.
**GIVEN** under my **HAND and SEAL of the COURT** this 10th day of NOVEMBER, 2021

R.B. MASSAM
DEPUTY REGISTRAR
ARUSHA

116604802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi……242/2021**

**Ombi la APATAE BOZENI JUMA kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehem BOZENI JUMA ISMAIL MLAHI.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja na kuhudhuria shaurini mnamo 7/9/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 26/11/2021

HAKIMU

116605902

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.185 OF 2021**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JENEPHA YOHANA MWILAWI**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY NEEMA DANIEL RAPHAEL**

**GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filled on or before the 14/12/2021.
Dated at Dodoma this 01/12/2021.

RESIDENT MAGISTRATE

116596402

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**MASHAKA EMMANUEL MKAMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1803/0135** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia LOWASSA SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/626803/2021.**

116604302

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JUSTINA WILLIAM EDWARD** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 826 BSK – NISSAN CARAVAN.** Chassis namba **CQGE2400607.** Engine namba **0032003993.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/570219/2021.**

116605102

---

## KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI

**HADIJA A NG'ADOA**
ANATANGAZA KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO LA KUMILIKI ARDHI YENYE **KUMB.NA.MG/MG/LD/17153** MMILIKI ALIOANDIKWA: ALLY SAIDI NG'ADOA **S.L.P 214 MOROGORO.** NA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU HADIJA ALLY NGADOA S.L.P 166, MOROGORO, NAMBA YA **SIMU: 0652944455**
ARDHI: KIWANJA NA.154 KITALU "A" MSAMVU MANISPAA YA MOROGORO
**MORO/MORO/RB/565017/2021**

KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

116605802

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SIMONI MUSSA SHEDAFA**
Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki (haujue) yenye namba za usajili **MC851BRR** yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0717196289**
**DSM /PHQ/RB/578723/2021**

116596302

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LAURENT VENANCE MSINZO** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye jina KAZIMOTO COMPLEX namba za usajili MC 421 BVJ aina ya BOXER.Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa cha Polisi. Taarifa ya Polisi.
**DOD/DOD/RB/576661/2021.**

116606502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**
**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU**
**WILAYA YA GEITA**
**SHAURI LA MADAI NA: 190/2021**
**MDAI: GROUP 12 SECURITY SERVICE LTD**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: GWANCHELE GREEN VIEW HOTEL WA**
**TANZANIA BARA NA VISIWANI**
**AMRI:**
Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 16/12/2021 saa 2:30 asubuhi bila kukosa. Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama leo JUMANNE tarehe 07 mwezi wa 12, 2021.

HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE
GEITA

116596202

---

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**OFISI ZA MATANGAZO**

**Mikocheni Industial Area,**

**Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Ethiopia yadai kuidhibiti miji miwili kutoka kwa waasi

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

SERIKALI ya Ethiopia imetangaza kuidhibiti tena miji miwili ya kimkakati ya Dessie na Kombolcha, mwezi mmoja baada ya kushikiliwa na wapiganaji wa Tigray.

Hatua hiyo ni ya hivi karibuni katika mfululizo wa ushindi wa haraka katika uwanja wa vita unaotangazwa na vikosi vitiifu vya Waziri Mkuu Abiy Ahmed.

Idara ya Mawasiliano ya serikali ilisema katika tangazo kupitia Twitter kwamba miji ya Dessie na Kombolcha, imekombolewa na vikosi vya usalama vya pamoja, ambavyo pia vilichukua udhibiti wa miji kadhaa upande wa mashariki.

Shirika la Utangazaji la Taifa Ethiopia, limemnukuu Waziri Mkuu Abiy akisema kwamba, waasi wameshindwa vibaya na hawakuweza kuhimili mashambulizi ya vikosi vya pamoja, akiongeza kuwa adui atashindwa na ushindi utaendelea kupatikana.

Waziri Mkuu Abiy, aliamua kungana na wanajeshi wake katika uwanja wa mapambano mwezi uliopita, baada ya wapiganaji wa Tigray kudai kuwa wanayashikilia maeneo makuu wakati wakizidi kusonga kuelekea mji mkuu wa Addis Ababa.

Serikali yake wiki iliyopita ilidai kwamba, jeshi lilidhibiti eneo la Lalibela, ambalo liliangukia mikononi mwa waasi mwezi Agosti na vilevile mji wa Shewa Robitambao, uliopo kilometa 220 kutoka Addis Ababa.

Msemaji wa TPLF, Getachew Reda aliandika kupitia Twitter juzi jioni kwamba, vikosi vya waasi vimeondoka katika miji ikiwamo Kombolcha na Dessie, kama sehemu ya mkakati.

Siku moja kabla kiongozi wake Debretsion Gebremichael, alikanusha madai ya serikali kupata ushindi mkubwa, akisema waasi walikuwa wakifanya marekebisho ya kimkakati na hawajashindwa.

Wakati huohuo, nchi sita ikiwamo Marekani zimeelezea wasiwasi juu ya ripoti za ukamataji mkubwa wa Watigrinya kwa kuzingatia misingi ya ukabila kuhusiana na mgogoro wa Tigray, uliodumu kwa mwaka mmoja na kuitaka serikali kukomesha vitendo vinavyotajwa kuwa ukiukaji wa sheria za kimataifa.

Nchi hizo zimenukuu ripoti za tume ya haki za binadamu ya Ethiopia na kundi la kimataifa la haki za binadamu Amnesty International, kuhusu kukamatwa kwa watu wengi wa kabila la Tigrinya, sambamba na padri wa kiorthodoksi, wazee na kinamama wenye watoto. **DW**



Vikosi vya usalama vya nchini Iraq, vikikagua gari lililoathiriwa na mlipuko wa bomu mjini Basra, jana na kuua watu wanne, huku Islamic State (IS) ikishukiwa kuhusika. **PICHA: REUTERS**

# Iran yabuni mpango madhubuti kukabili vikwazo dhidi nchi yake

**Dar es Salaam,** TANZANIA

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, Hossein Amir-Abdollahian, amesema nchi yake imebuni mpango madhubuti wa kuondoa vikwazo sambamba na mpango wa maendeleo endelevu kiuchumi.

Hayo yalibainishwa juzi katika taarifa yake, iliyotolewa na Kituo cha Utamaduni cha Iran, hapa nchini kwa vyombo vya habari.

Alisema mwelekeo kwa awamu sita za mazungumzo ya Vienna hayakuleta mafanikio, kutokana na madai ya kupindukia ya Marekani na misimamo isiyo ya kweli.

"Sasa tunaanza duru mpya ya mazungumzo, lengo kuu la mazungumzo hayo ni kurejesha haki za taifa la Iran na kuondolewa vikwazo vyote vilivyowekwa Iran kwa upande mmoja na nje ya mipaka yake na Marekani ambayo si mshirika wa Mpango wa Pamoja wa Utekelezaji (JCPOA) tangu Mei, 2018.

Alisema Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, licha ya kutofanya kazi kwa kiasi kikubwa kwa nchi za Magharibi katika JCPOA, iko tayari tena, kwa nia njema, kwa mazungumzo yenye matokeo ili kufikia sehemu nzuri na ina imani na azma ya kufikia makubaliano mazuri huko Vienna.

"Azimio nambari 2231 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linazitaka nchi zote wanachama kuchukua hatua zinazofaa ili kuunga mkono utekelezaji wa JCPOA, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua zinazolingana na mpango wa utekelezaji ulioainishwa katika JCPOA na azimio hili na kujizuia kutokana na hatua zinazodhoofisha utekelezaji wa ahadi chini ya JCPOA.

"Ningependa kusisitiza kwa mara nyingine kwamba fursa hii si dirisha ambalo linaweza kubaki wazi milele na Marekani na nchi tatu za Ulaya lazima zilielewe hili vizuri.

Alisema timu ya mazungumzo ya nyuklia ya Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, inashiriki kikamilifu na kwa dhati katika mazungumzo ya Vienna kwa nia njema, ikifuata mantiki ya mazungumzo ambayo yanalinda maslahi na haki za taifa la Iran.

## Polisi aua mke, wengine watano, ajiua

**Nairobi,** KENYA

POLISI nchini Kenya, amemuua mke wake na kuua watu wengine watano kabla ya kujiua.

Tukio hilo la kusikitisha limesababisha vifo vya watu saba, wakiwamo majirani na waendesha bodaboda, Kamanda wa Polisi wa Kaunti ya Kabete, Francis Wahome, alithibitisha.

Majibizano ya risasi yalisikika majira ya alfajiri katika eneo la nyumba ya ghorofa na soko.

Muda mfupi baada ya saa sita usiku, ofisa huyo akiwa na bunduki aina ya AK 47, alivamia na kumuua mkewe na wengine watano wakiwamo waendesha bodaboda wawili, mmoja kati yao, anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Taifa ya Kenyatta.

Wakazi wa ghorofa hilo, walisema walisikia kishindo kikubwa kutoka kwa nyumba ya wanandoa hao usiku wa manane.

Dakika chache baadaye, waliripoti kile kilichoonekana kama moto kutoka kwa nyumba hiyo hiyo na kuripoti tukio hilo katika Kituo cha Polisi cha Kabete.

Walipofika, maofisa kutoka kituo hicho waligundua kuwa polisi huyo alimuua mkewe kwa kumpiga risasi na kwamba baadaye alienda kwenye mashambulizi ya risasi ambayo yalisababisha vifo zaidi.

Haikuweza kufahamika mara moja ni nini kilisababisha kurushiana risasi kwa ofisa huyo. **BBC**

## WHO yaonya waliopona corona kuchangia damu

**Geneva,** USWISI

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limewashauri wale wote waliougua Covid-19 na kupona, kutochangia damu hususan kwa wagonjwa wanaougua ugonjwa huo, kutokana na utafiti kuonyesha damu hiyo haimsaidii mgonjwa.

Ushauri huo umetolewa na WHO, baada ya jopo lake la kimataifa la wataalamu wa miongozo kuchambua matokeo ya majaribio 16, yaliyohusisha wagonjwa 16,236 ambao wana maambukizi na hawako mahututi na wale wagonjwa wa Covid-19 walio mahututi.

Hatua za wali za utafiti huo, zilionyesha matumaini, utafiti wa sasa unaonyesha dhahiri kwamba mtu aliyeugua na kupona ugonjwa huo, akimwongezea damu mgonjwa anayeugua haimsaidii kupata nafuu.

Pia ripoti ilisema mgonjwa anayeugua ugonjwa huo, hawezi kupunguza uhitaji wake wa kuwekwa kwenye mashine ya kusaidia kupumua na zaidi ya yote unaongeza gharama na kuchukua muda mrefu kumwekea damu mgonjwa.

WHO imepinga vikali matumizi ya damu kwa mtu aliyeugua na kupona kuwekewa wagonjwa wanaougua sasa wasio mahututi na wale walio mahututi, isipokuwa damu hiyo inaweza kutumika katika muktadha wa kufanya majaribio yaliyodhibitiwa bila mpangilio kwa kitaalamu ukifahamika kama RCT. **UN**

HABARI MICHEZO

# KUZIONA STARS, UGANDA CRANES BUKU 2 KWA MKAPA

**Na Saada Akida**

TIMU za Taifa za Tanzania, Taifa Stars na Tanzanite zitashuka dimbani kesho dhidi ya Timu ya Taifa ya Uganda 'The Cranes' wanaume na wanawake, katika mchezo wa kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru huku viingilio kushuhudia mechi hizo vikiwa ni Sh. 2,000 kwa 5,000 tu, imeelezwa.

**Michezo hiyo ya kirafiki itaanza kupigwa saa 11:00 jioni kwa timu ya Twiga Stars ikiwakaribisha timu ya Taifa ya Wanawake Uganda na kisha kufuata mechi ya Taifa Stars dhidi ya The Cranes saa 2:00 usiku, zote zikipigwa katika Uwanja wa Benjamini Mkapa.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Slaam jana, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Yusuph Singo, alisema tayari timu za Tanzania zimeingia kambini na zinaendelea vizuri na maandalizi ya michezo hiyo.

Alisema timu hizo za Uganda zitawasili nchini leo tayari kwa mechi hizo za kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru, ambazo zitafanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Maandalizi yanaendelea vizuri na tunatarajia mechi hizo zitachezwa jioni kuanzia saa 11:00, kwa wanawake na Taifa Stars itacheza saa 2:00 usiku dhidi ya The Cranes," alisema Singo.

Singo aliwataka Watanzania kujitokeze kwa wingi kusapoti timu za Tanzania kwa sababu viingilio ni rafiki na kila Mtanzania anaweza kununua tiketi ili kuingia uwanjani kushuhudia timu zao zikicheza mechi hizo za kirafiki.

Alivitaja viingilio vya mchezo huo kuwa mzunguko ni Sh. 2,000 na Sh. 5,000 tu kwa VIP A na B.

Wachezaji wa Taifa Stars walioitwa kwa ajili ya mechi hiyo ni Metacha Mnata (Polisi Tanzania), Haroun Mandanda (Mbeya City), Musa Mbisa (Coastal Union), Nathaniel Chilambo (Ruvu Shooting), Kelvin Kijiri (KMC), Hans Masoud (Coastal Union), Nickson Kibabage (KMC) na Oscar Masai wa Geita Gold.

Wengine ni Abdulrazack Mohamed (KMC), Lusajo Mwaikenda (Azam), Abdulmajid Mangalo (Biashara United), Nashon Naftali (Geita Gold), Tariq Simba (Polisi Tanzania), Sospeter Bajana (Azam), Hassan Nassor (Dodoma Jiji) na Abdul Hamis Suleiman kutoka Coastal Union.

Wachezaji wengine ni Meshack Abraham (Kagera Sugar), Cleophace Mkandala (Dodoma Jiji), Denis Nkane (Biashara United), Rashid Juma (Ruvu Shooting), Vitalis Mayanga (Polisi Tanzania), Anuary Jabir (Dodoma Jiji) pamoja na Reliants Lusajo wa Namungo FC.



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa na baadhi ya viongozi wa timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kwa Watu wenye Ulemavu baada ya kuzungumza nao jana katika Viwanja vya Ikulu jijini Dar es Salaam. **PICHA: IKULU**

# *Tigo yatia neno Kilimanjaro Marathon*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo, ambayo inadhamini mbio za Km. 21 za Kilimanjaro Marathon, imetoa wito kwa washiriki wa kinyang'anyiro hicho kwenda kujisajili kwa wingi wakati huu zikiwa zimebaki takriban miezi miwili na nusu kabla ya kufanyika mashindano hayo maarufu mjini Moshi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael, alitoa wito kwa washiriki kutumia fursa ya punguzo la asilimia 20 kujisajili ili kuepusha usumbufu dakika za mwisho.

"Maandalizi yamepamba moto na usajili unaendelea, tunawaomba watumie Tigo Pesa kujisajili kwa kubonyeza *149*20# kisha wataulizwa maswali machache ili kukamilisha usajili baada ya kulipia," alisema Woinde.

Aliendelea kueleza kuwa, kwa mujibu wa waandaaji punguzo la bei hiyo litaendelea hadi Januari 7, mwakani ambapo bei zitapanda.

Alisema Tigo inaendelea na maandalizi vizuri ili kuwapa washiriki wenye uzoefu kamili na kuhakikisha kuwa mbio za Km. 21 zinaendelea kuwa maarufu wakati mbio za Kilimanjaro Marathon zikiadhimisha miaka 20 mwakani.

"Huu ni mwaka wetu wa saba tangu tuanze kudhamini mbio hizi na msukumo mkubwa ni namna mbio hizi zinavyohamasisha utunzaji wa mazingira katika Mlima Kilimanjaro ili kuhakikisha theluji ya mlima huo haiyeyuki. Namna mbio hizo zinavyokuza vipaji, utalii na biashara kwa ujumla katika Mkoa wa Kilimanjaro na mikoa jirani unakua pia," alisema.

Alibainisha kuwa Tigo pia itaendelea na kampeni ya upandaji miti maarufu kama 'Tigo Green for Kili.'

Wadhamini wengine wa mbio hizo ni pamoja na Kilimanjaro Premium Lager wanaodhamini mbizo za Km. 42, Grand Malt (Km. 5), Unilever, TPC Sugar, Simba Cement, Kilimanjaro Water huku meza za maji wadhamini wakiwa ni Absa, wasambazaji maalumu Kilimanjaro Leather Industries Company Limited, GardaWorld Security, Keys Hotel, Kibo Palace Hotel na CMC Automobiles.

## Mbeya City yazipiga bao Simba, Yanga

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbeya City imefikisha mechi ya nane mfululizo za Ligi Kuu bila kupoteza, ikipaa hadi nafasi ya tatu kwa kufikisha pointi 14, baada ya ushindi wa mabao 2-0 juzi dhidi ya Dodoma Jiji, hivyo kuzipiku Simba na Yanga ambazo zimecheza mechi saba bila kupoteza.

Simba na Yanga zinatarajiwa kucheza Jumamosi na ili zote kuweza kufikia rekodi hiyo ya Mbeya City, labda mechi hiyo imalizike kwa sare, vinginevyo moja ikifungwa itaendelea kufunikwa na miamba hiyo ya Mbeya.

Mbeya City, ambayo ni kama imekuwa ikifukuza mwizi kimya kimya, imekuwa ni timu isiyoongelewa sana, lakini ni moja kati ya timu tatu ambazo hazijapoteza mechi yoyote ya Ligi Kuu mpaka sasa, zikiwamo Simba na Yanga.

Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, ameonyesha kufurahishwa na ushindi wa mabao 2-0 ambao timu yake imeupata Uwanja wa Sokoine Mbeya, akisema wamejifunza kwenye mechi iliyopita walipokuwa wakiruhusu mabao yao kurudishwa.

## Harerimana kusajili wanne dirisha dogo

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mbeya Kwanza, Haruna Harerimana, amesema tayari ameona udhaifu wa kikosi chake na kufanyia kazi baadhi ya maeneo, hivyo kilichobaki sasa ni kufanya usajili wa nafasi nne wakati dirisha dogo litakapofunguliwa Desemba 15, mwaka huu ili kukiboresha zaidi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Harerimana alisema kulingana na ugumu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, anahitaji kufanya maboresho katika kikosi chake ili kupambana kutafuta matokeo mazuri katika michezo iliyo mbele yao.

"Baada ya hizi mechi chache kuona mapungufu yetu, tunatakiwa kuboresha zaidi kikosi ikiwamo kupata wachezaji ambao watacheza nafasi hizo na watalete ushindani kwa waliopo.

"Katika msimamo tuko kwenye nafasi mbaya na tunatakiwa kupambana kutafuta matokeo mazuri mechi zilizopo mbele yetu, lakini kuboresha kikosi katika nafasi hizo," alisema Harerimana ambaye timu yake hiyo ipo nafasi ya 14, baada ya mechi nane hadi sasa.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### AZPILICUETA KUTUA BARCA

MLINZI wa Chelsea, Cesar Azpilicueta, 32, anafanya mazungumzo na Barcelona juu ya uhamisho msimu huu. ***(El Nacional, via Daily Mail)***

#### ATAKIWA NEWCASTLE



KOCHA wa Newcastle, Eddie Howe, amemworodhesha katika nyota anaowataka mshambuliaji wa Stoke City, Tyrese Campbell, 21. ***(Sun)***

#### DEMBELE AWINDWA UNITED

KLABU ya Manchester United imeungana na Newcastle United katika kumsaka winga wa Barcelona, Ousmane Dembele, 24, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, akiwa amefanya uamuzi juu ya hali yake ya baadaye. ***(Mundo Deportivo, via Express)***

#### MEE KUONGEZEWA MSHAHARA




KLABU ya Newcastle inajiandaa kuongeza mshahara mara dufu kwa mlinzi wa klabu ya Burnley, Ben Mee, 32 na James Tarkowski, 29, kujaribu kuwashawishi kujiunga na Newcastle. ***(Mirror)***

#### RANGNICK AMTAKA JONG




KOCHA mpya wa Manchester United, Ralf Rangnick anafuatilia kwa karibu kwa lengo la uhamisho wa kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong, 24, ambaye kwa sasa yuko Barcelona huku akianza mchakato wa kujenga upya kikosi chake pale Old Trafford. ***(El Nacional, via Daily Star)***

#### SZALAI AKARIBIA FENERBAHCE




HATUA ya Chelsea ya kumchukua mlinzi wa Fenerbahce, 23, Attila Szalai ni "mpango uliokamilika", kwa mujibu wa kocha Marco Rossi. ***(Mirror)***

#### KUMKOSA ELYOUNOUSSI




WINGA wa Norway ambaye analengwa na Arsenal, Mohamed Elyounoussi mwenye umri wa miaka amesisitiza kuwa yeye na familia yake wanafurahia maisha katika klabu ya Southampton. ***(Sun)***

#### IBRAHIMOVIC ANOGEWA MILAN



MSHAMBULIAJI wa AC Milan, Msweden Zlatan Ibrahimovic, 40, ameelezea matamanio yake ya kuendelea kubakia katika klabu hiyo ya Serie A. ***(Star)***

#### DALOT KUBAKI UNITED



MLINZI wa Ureno, Diogo Dalot, 22, amekuwa akitoa jumbe za kusisitiza kuwa yuko tayari "kutoa kila kitu" kwa Manchester United katika kile kinachoonekana kuwa ni pigo kwa klabu nyingine zinazomtaka. ***(Daily Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: KAZI BADO

Ninachotaka ni zaidi kutoka kwa timu yangu, leo (juzi), mchezo haukuwa mzuri kwetu na lazima...

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amekubali 'Washikabunduki' hao hawakuwa vizuri vya kutosha kwani waliteseka kwa dakika za lala salama dhidi ya Everton kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, juzi Jumatatu wakati wakifungwa mabao 2-1.

**Arsenal ya Arteta ilipata kipigo chake cha tatu katika mechi nne za Ligi Kuu msimu huu baada ya juhudi nzuri za Demarai Gray kuona wenyeji wakinyakua ushindi huo mnono dakika ya 92.**

Martin Odegaard alikuwa amewapa wageni bao la kuongoza kwa muda wa mapumziko kwa pasi kutoka kwa Kieran Tierney katika Uwanja wa Goodison Park.

Richarlison alisawazisha kabla ya Gray kukamilisha mabadiliko katika dakika ya pili ya muda wa mapumziko.

Arteta anahisi wachezaji wake waliadhibiwa kwa kukosa umakini wa mchezo baada ya kushindwa mara tatu mfululizo kwenye ligi na Everton kwa mara ya kwanza tangu 1986.

"Katika kipindi cha kwanza, tulikuwa hatuendani na mpira," Arteta aliiambia Sky Sports.

"Sikupenda. (Hatukuwa na) uwezo wa kupenya, mara chache tulipofanya hivyo, tulifunga.

"Kipindi cha pili, tulijaribu kufanya zaidi, tukatengeneza nafasi nne kubwa, lakini tukaruhusu bao la ovyo.

"Ninachotaka ni zaidi kutoka kwa timu yangu. Leo (juzi), mchezo haukuwa mzuri kwetu na lazima utafute njia ya kushinda.

"Ingeweza kuwa tofauti sana, lakini hatujaweza kufanya hivyo."

Odegaard alikubaliana na Arteta kwamba Arsenal walio katika nafasi ya saba lazima waboreshe kiwango chao cha uchezaji.

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 761

MECHI KALI
HOME
AWAY
MANCHESTER UTD
1.44 | 4.68 | 6.55
BSC YOUNG BOYS

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# KLOPP AZUNGUMZIA MKATABA WA SALAH

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Jurgen Klopp amekiri kuwa uvumilivu unahitajika huku Liverpool wakiendelea kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na Mohamed Salah.

Mkataba wa sasa wa Salah na 'Wekundu' hao unamalizika Juni 2023 na mustakabali wake umekuwa gumzo kwa muda mrefu.

Mshambulizi huyo mahiri ametangaza kwamba, anataka kubaki Anfield, lakini hakuna makubaliano ambayo yamefikiwa kati ya klabu hiyo na mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri. Inasemekana kwamba, Salah aliiambia MBC Masr TV kwamba mustakabali wake uko "mikononi mwa wasimamizi na wanapaswa kutatua suala hili".

Klopp Jumatatu alisema kuwa msimamo wa klabu hiyo haujabadilika.

Alisema katika mkutano na waandishi wa habari usiku wa kuamkia mechi ya Ligi ya Mabingwa huko Milan: "Tunajua hasa anachohusu na tunazungumza.

"Kuongeza mkataba na mchezaji wa aina ya Mo si jambo unalofanya pale mnakutana kwa kikombe cha chai mchana na kupata muafaka, hilo ni jambo la kawaida kabisa.

"Kwa kweli hakuna kitu kingine cha kusema juu ya Mo. Anazungumza juu yake wakati anaulizwa juu yake, naweza kusema machache tu kwa sababu mengine yote si ya umma.

# *Perisic njiapanda Inter*

**MILAN,** Italia

WINGA wa Inter Milan, Ivan Perisic, hatazungumzia mustakabali wake kwa "wiki kadhaa".

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia ana mkataba hadi mwishoni mwa msimu huu na imeripotiwa kuwa Kocha wa Tottenham, Antonio Conte, anataka kuungana tena na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32.

Perisic, ambaye amefunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho mbili katika mechi 19 msimu huu, anasema anavutiwa tu na nia ya mabingwa wa Serie A, Inter kushinda mataji zaidi kwa sasa.

Alisema katika mkutano na waandishi wa habari siku ya Jumatatu: "Miaka miwili iliyopita imekuwa ya ajabu kwangu, lakini hii ni siku zilizopita.

"Nina njaa, tunataka kushinda tena mwaka huu." "Tuna wakati na katika wiki kadhaa tutazungumza (kuhusu mustakabali wake). Hebu tuone nini kinaweza kutokea."



## HABARI MICHEZO


,374,640

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/12/21 | 18:00 | Peterborough vs Millwall | 3.04 | 3.19 | 2.29 |
| 02. 11/12/21 | 18:00 | Derby vs Blackpool | 2.34 | 3.14 | 2.99 |
| 03. 11/12/21 | 18:15 | Alaves vs Getafe | 2.37 | 2.94 | 3.34 |
| 04. 11/12/21 | 23:00 | Athletic Bilbao vs Sevilla FC | 2.64 | 3.09 | 2.79 |
| 05. 12/12/21 | 14:30 | Torino vs Bologna | 2.30 | 3.25 | 3.15 |
| 06. 12/12/21 | 15:00 | Lille vs Lyon | 2.50 | 3.49 | 2.65 |
| 07. 12/12/21 | 17:00 | Brighton vs Tottenham | 3.00 | 3.20 | 2.42 |
| 08. 12/12/21 | 17:00 | Metz vs Lorient | 2.35 | 3.28 | 2.99 |
| 09. 12/12/21 | 19:00 | Strasbourg vs Marseille | 2.64 | 3.34 | 2.59 |
| 10. 12/12/21 | 19:30 | Crystal Palace vs Everton | 2.27 | 3.20 | 3.25 |
| 11. 12/12/21 | 20:00 | Sassuolo vs Lazio | 2.89 | 3.49 | 2.34 |
| 12. 12/12/21 | 20:15 | Alcorcon vs FC Cartagena | 2.94 | 2.94 | 2.50 |
| 13. 12/12/21 | 20:30 | Betis vs Real Sociedad | 2.35 | 3.25 | 3.05 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 08 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 2397 | Prison Leopards vs Konkola Blades | 2.31 | 2.70 | 3.38 |
| 16:00 | 2593 | Red Arrows vs Kabwe Warriors | 2.39 | 2.69 | 3.22 |
| 16:00 | 3811 | Al-Sailiya SC vs Al Gharafa SC | 4.83 | 4.06 | 1.55 |
| 16:00 | 5360 | Lusaka Dynamos vs Zesco United | 3.80 | 2.74 | 2.12 |
| 16:00 | 5385 | Power Dynamos vs Kansanshi Dynamos | 1.44 | 3.61 | 7.70 |
| 16:00 | 5586 | Nkwazi vs Indeni FC | 1.96 | 2.90 | 4.06 |
| 16:00 | 5806 | Tenisca vs CD Tenerife B | 2.29 | 3.09 | 2.95 |
| 16:30 | 3059 | Mamelodi Sundowns vs Bloemfontein Celtic | 1.43 | 4.22 | 6.87 |
| 16:45 | 2564 | Persib Bandung vs Persebaya Surabaya | 1.75 | 3.31 | 4.42 |
| 17:00 | 3222 | Hyderabad FC vs Bengaluru FC | 2.10 | 3.28 | 3.13 |
| 17:20 | 3837 | Kazma SC vs Al Shabab Kuwait | 1.64 | 3.66 | 4.62 |
| 17:25 | 3641 | AL Nahdha vs AL Draih | 2.06 | 3.14 | 3.38 |
| 17:30 | 2349 | AL Adalh vs Alshoulla | 2.32 | 2.94 | 3.04 |
| 18:00 | 3054 | Cfc-Cf Canelas 2010 vs AD Sanjoanense | 2.29 | 3.09 | 2.94 |
| 18:00 | 3505 | AD Fafe vs Anadia FC | 1.93 | 3.04 | 3.96 |
| 18:00 | 4034 | SC Vianense vs Maritimo B | 3.65 | 3.55 | 1.99 |
| 18:00 | 4678 | Atzeneta UE vs Atletico Saguntino | 2.19 | 2.89 | 3.37 |
| 18:00 | 4777 | Baroka FC vs Moroka Swallows FC | 2.64 | 2.74 | 2.98 |
| 18:00 | 5079 | Stellenbosch vs SuperSport Utd | 2.89 | 2.94 | 2.54 |
| 18:00 | 5422 | Sekhukhune United vs Tshakhuma | 2.46 | 2.76 | 3.20 |
| 18:10 | 2987 | Al Arabi Doha SC vs Qatar SC | 1.83 | 3.61 | 3.61 |
| 18:30 | 3320 | Amazulu vs Orlando Pirates | 2.90 | 2.80 | 2.65 |
| 18:45 | 3923 | Vllaznia vs Partizani Tirana | 2.25 | 3.05 | 3.45 |
| 18:45 | 4764 | Skenderbeu vs Egnatia Rrogozhine | 2.25 | 3.10 | 3.40 |
| 19:00 | 1606 | Barakaldo vs Pasaia KE | 2.05 | 3.09 | 3.48 |
| 19:00 | 1711 | HNK Rijeka vs NK Osijek | 2.22 | 3.28 | 2.90 |
| 19:00 | 2461 | Felgueiras vs CDC Montalegre | 2.18 | 2.94 | 3.33 |
| 19:00 | 2793 | NK Celje vs Olimpija Ljubljana | 2.65 | 2.70 | 2.84 |
| 19:00 | 3281 | Felanitx vs Santanyi | 3.51 | 3.03 | 2.06 |
| 19:00 | 4568 | SD Deusto vs Leioa | 2.41 | 2.95 | 2.90 |
| 19:00 | 5042 | UD San Pedro vs CF Malaga B | 3.62 | 3.09 | 2.00 |
| 19:35 | 3161 | Al Fehahee vs AL Arabi | 4.83 | 3.82 | 1.58 |
| 20:30 | 2932 | Golden Arrows vs Kaizer Chiefs | 1.96 | 3.19 | 3.88 |
| 20:45 | 4001 | Zenit St Petersburg vs Chelsea | 5.79 | 4.29 | 1.53 |
| 20:45 | 5136 | Juventus vs Malmo | 1.21 | 6.22 | 13.32 |
| 21:00 | 1525 | Alverca Futebol vs Vitoria Setubal | 2.55 | 3.23 | 2.51 |
| 21:00 | 2910 | FSV Luckenwalde vs Lokomotive Leipzig | 3.32 | 3.51 | 1.94 |
| 22:45 | 2287 | Livingston vs Hibernian | 3.26 | 3.16 | 2.21 |
| 22:45 | 3101 | Bradford City vs Colchester | 1.68 | 3.63 | 4.81 |
| 22:45 | 3430 | MK Dons vs Plymouth | 2.22 | 3.38 | 2.99 |
| 22:45 | 3655 | Barrow vs Salford City | 2.54 | 3.18 | 2.69 |
| 22:45 | 4085 | Wigan vs Shrewsbury | 1.62 | 3.77 | 5.09 |
| 22:45 | 5163 | Hartlepool vs Rochdale | 2.68 | 3.27 | 2.49 |
| 23:00 | 2061 | Bayern Munchen vs Barcelona | 1.64 | 4.50 | 4.40 |
| 23:00 | 2340 | Benfica vs Dynamo Kiev | 1.33 | 5.19 | 8.78 |
| 23:00 | 3001 | Atalanta vs Villarreal | 1.73 | 4.09 | 4.19 |
| 23:00 | 4426 | RB Salzburg vs Sevilla FC | 3.01 | 3.36 | 2.33 |
| 23:00 | 4497 | VfL Wolfsburg vs Lille | 2.29 | 3.34 | 3.09 |
| 23:00 | 4538 | Berazategui vs Argentino Merlo | 2.21 | 3.14 | 3.04 |
| 23:00 | 5002 | Manchester Utd vs BSC Young Boys | 1.44 | 4.68 | 6.55 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# TAMASHA LA 'TWENZETU KILIMANJARO' LAIVA

**Na Mwandishi Wetu**

WENYEJI na wageni wanaotarajiwa kutembelea Mkoa wa Kilimanjaro kwa ajili ya mapumziko ya mwishoni mwa mwaka, wameandaliwa burudani mbalimbali kwenye tamasha kubwa linalojulikana kama 'Twenzetu Kilimanjaro' linalotarajiwa kufanyika Desemba 26, mwaka huu, katika Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka na Hoteli ya Marangu, mkoani humo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mratibu wa Tamasha hilo kutoka Kampuni ya Real PR Solutions, Irene Lyimo, alisema tamasha hilo ni sehemu ya mkakati wa kufanikisha mpango wa kuendeleza utalii wa ndani na linatarajiwa kupambwa na matukio mbalimbali ikiwamo maonyesho ya Utalii na Biashara, Burudani na viburudisho mbalimbali ikiwamo vyakula vya asili, michezo ya watoto pamoja na muziki huku likitarajiwa kuhusisha mbio za kujifurahisha.

"Mbio hizo zitahusisha kilometa tano, Km. 10 pamoja na mbio za baiskeli za Km. 42, zinazotarajiwa kuanza majira ya saa 12:00 asubuhi.

"Pia, siku tatu kabla ya mashindano hayo (Desemba 23) kutakuwa na zoezi la kutoa misaada mbalimbali kwenye huduma za afya Kibosho na Marangu, na mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro atawaongoza wafanyakazi wa umma, viongozi mbalimbali pamoja na wananchi, kutoa misaada kwenye hospitali zetu.

"Tunatumia fursa hii kuwaomba wafanyakazi pamoja na watumishi wengine kutika mikoa hiyo, kujisajili katika mbio hizo pamoja na shughuli nyingine zinazoambatana na tamasha hili la Twenzetu Kilimanjaro mwaka 2021 ikiwamo utoaji msaada katika hospitali zetu," alisema.

Akizungumzia zaidi kuhusu mbio za Capital Mountain Run zitakazopamba tamasha hilo, mtaalamu wa mbio hizo, Joshua Kayombo, alisema kwa kuwa tamasha hilo linalenga kutangaza utalii ili kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan, njia zitakazotumika zinazohusisha maeneo yenye vivutio ili kutoa nafasi kwa washiriki kupata fursa ya kujionea mandhari nzuri za asili katika mkoa huo.

"Mbio hizi zitafanyika kwa wakati mmoja katika maeneo mawili tofauti yaani Marangu Hoteli na Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka kilichoko Kibosho. Baada ya mbio hizi washiriki watapata fursa ya kuendelea na burudani mbalimbali kwa ajili yao na familia zao ikiwamo vyakula vya asili, ngoma za asili na vinywaji mbalimbali," alisema.

Akizungumzia kuhusu usafiri wa kuelekea kwenye tamasha hilo kutokea jijini Dar es Salaam na kurudi, Mkurugenzi wa Kampuni inayotoa huduma za usafiri wa abiria ya Wonderland Afrika, Saidi Lukemo, alisema wamejipanga kuhakikisha washiriki wanapata usafiri wa uhakika kwa bei nafuu kuanzia Desemba 24 na kurudi Desemba 27, mwaka huu, baada ya tukio hilo.




Mratibu wa Tamasha la Twenzetu Kilimanjaro, Irene Lyimo (kulia), sambamba na mtaalamu wa mbio zitakazopamba tamasha hilo zinazofahamika kama Capital Mountain Run, Joshua Kayombo (katikati) pamoja na mwakilishi wa wadau wa mbio hizo kutoka Kampuni ya Matangazo ya A1 Outdoor, Cassandra James, wakionyesha medali na fulana maalum zitazotolewa kwa washiriki wa mbio hizo zinazotarajiwa kufanyika Desemba 26, mwaka huu, katika Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka na Hoteli ya Marangu mkoani Kilimanjaro, zikilenga kutangaza utalii wa ndani. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Mbombo aipania Kagera Sugar*

**Na Dennis Fussi**

TIMU ya Azam FC, imedhamiria kuirarua Kagera Sugar katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kesho, Alhamis katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es salaam.

Azam iliyoanza kurejea kwenye makali yake, baada ya kuanza Ligi Kuu msimu huu kwa kusuasua, imeonyesha dhamira hiyo kupitia kwa mshambuliaji wake kutoka DR Congo, Idriss Mbombo.

Mbombo ambaye alifunga bao la ushindi kwenye mchezo uliopita dhidi ya Mtibwa Sugar, amesema wamejipanga kuwamaliza Kagera Sugar kwenye mchezo huo ili kuipa timu yao alama tatu muhimu.

"Kikubwa kuelekea kwenye mchezo wetu, maandalizi yapo sawa na tunahitaji kupata alama tatu ili kuweza kuendelea kwenye kasi yetu ambayo tumeanza nayo," alisema.

Azam imeshajikusanyia alama 10 zinazoiweka katika nafasi ya saba katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu wa 2021/22, huku Kagera Sugar ikishika nafasi ya 12 kutokana na alama zake nane.

# Michezo

Jumatano Desemba 8, 2021

Nipashe




Arteta: Kazi bado Arsenal

UKURASA 21

KAFANYENI KWELI...



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Tanzania ya Watu wenye Ulemavu 'Tembo Warriors', wakimsikiliza kwa makini Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, wakati akizungumza nao katika hafla ya kuwapongeza pamoja na viongozi wao baada ya kufuzu kushiriki fainali za Kombe la Dunia kwa Watu wenye Ulemavu 2022 nchini Uturuki. Hafla hiyo iliyoambatana na chakula cha mchana ilifanyika Viwanja vya Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Rais Samia aituma kazi Tembo Warriors Uturuki

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ameitaka Timu ya Taifa ya Tanzania ya Watu wenye Ulemavu, 'Tembo Warriors', ikaendeleze moto uleule Kombe la Dunia nchini Uturuki, kama iliyouonyesha kwenye michuano ya mpira wa miguu ya Afrika (CANAF), iliyomalizika wiki iliyopita hapa nchini.

Katika michuano hiyo ya CANAF, Tanzania ilikata tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia kwa wenye Ulemavu mwakani nchini Uturuki baada ya kutinga nusu fainali sambamba na Angola, Liberia na Ghana ambayo ilitwaa ubingwa huo.

Akizungumza kwenye hafla aliyoiandaa ya kuwapongeza wachezaji wa Tembo Warriors, benchi la ufundi na viongozi wao, Ikulu jijini Dar es Salaam jana, Rais Samia alisema kitendo cha timu hiyo kufuzu kwenda kucheza Kombe la Dunia kwa watu wenye ulemavu ni sifa kubwa kwa taifa na kuwataka kwenda pia kuipeperusha vema bendera ya Tanzania nchini Uturuki ambako fainali hizo zitafanyika Oktoba mwakani.

"Nendeni mkafanye kama ndiyo kwanza mnaanza, mafanikio haya yasiwafanye mjione sisi ndiyo sisi, mnakokwenda ni ugenini, huko nako kuna saikolojia yake, hapa mlishangiliwa vizuri kwa sababu mlikuwa na mashabiki, huko hakuna. Mimi nitakuwa pamoja nanyi, nitawapa mlezi mzuri wa kuwasimamia," alisema Rais Samia akiwaasa na kuwakumbusha nini wanatakiwa kwenda kufanya kwenye fainali hizo.

# Simba, Yanga 'litakufa jitu'

**Na Waandishi Wetu**

### ●●● Pablo awatoa wachezaji presha, Nabi yeye amtaja Fei Toto, Aucho, asema...

ZIKIWA zimesalia siku mbili kabla ya Jumamosi mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga kupigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, kwa namna tambo zilivyotawala huenda kuna timu itakufa kwa mabao mengi.

**Wakati klabu ya Yanga ikisema kuwa inajiamini kutokana na kuwa na kikosi kizuri zaidi, Simba imesema imejipanga kupata ushindi kwenye mechi hiyo.**

Ofisa Habari wa klabu ya Yanga, Hassan Bumbuli alisema kuwa kikosi chao kilianza rasmi mazoezi ya gym Jumatatu asubuhi na jioni wakahamia mazoezi ya uwanjani, tayari kwa ajili ya mechi hiyo.

"Hali inakwenda vizuri, lakini hatujiamini kama tunakwenda kushinda mechi hiyo, hapana, ila tunajimini kwa sababu tunakikosi kizuri ambacho kinaweza kutupa matokeo ya ushindi. Kocha Mkuu Nasreddine Nabi aliwapa mapumziko vijana wetu baada ya mechi ya Mbeya Kwanza, Ijumaa wakarejea, Jumamosi tukacheza mechi ya kirafiki dhidi ya Friends Rangers na tukashinda bao 1-0, na wachezaji waliocheza mechi hii ni wale ambao hawakucheza mechi ya Mbeya na kwa kifupi tu ni kwamba hatuna majeruhi kwenye kikosi chetu," alisema Bumbuli.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameliambia Nipashe kuwa mbali ya ubora wa wachezaji wake kwenye maeneo mengine kama Feisal Salum, Yannick Bangala, Khalid Aucho, Djigui Diarra wanaotazamwa kutoa burudani, lakini bado anahitaji kujiimarisha zaidi kuelekea mchezo huo.

"Kama nilivyosema awali kwamba hakuna mechi iliyo rahisi kwetu, tunatakiwa kujiimarisha zaidi katika kila idara hasa safu ya ulinzi na ushambuliaji kulingana na tulivyoona ubora wa wapinzani wetu," alisema Nabi.

Wakati Yanga ikisema hayo, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco yeye amesema ameridhishwa na namna wachezaji wake wanavyojiandaa na mchezo huo, lakini kurejea kwa kiungo mkabaji Thadeo Lwanga aliyekuwa akiuguza majeraha ya goti.

"Sisi tunaendelea na maandalizi yetu, mchezo dhidi ya Yanga ni kama michezo mingine, nafahamu katika nchi yoyote mchezo wa dabi unavuta hisia za watu wengi na wenye upinzani, lakini hatutaki kulichukulia hilo ndani ya uwanja, tutapambana kama tunacheza mechi nyingine na hatuna sababu ya kuwapa wachezaji presha," alisema Pablo.

Naye Ofisa Habari Msaidizi wa Klabu ya Simba, Ally Shatry maarufu 'Chico', alisema kikosi cha Simba kilitarajiwa kurejea jana jioni kutoka nchini Zambia, tayari kwa ajili ya mechi hiyo.

"Tunajua ni mechi ngumu, ni 'dabi', lakini tutaingia kama tunakwenda kucheza mechi nyingine yoyote ya Ligi Kuu, nia ni kusaka pointi tatu ili kujiweka vizuri kwenye msimamo wa ligi kwa sababu lengo letu ni ubingwa," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again' amewatoa hofu wanachama na mashabiki wa Simba kuelekea mechi hiyo ya Jumamosi, akisema bado wana timu nzuri inayoweza kupambana na timu yoyote ile, huku akiichukulia mechi hiyo ya 'dabi' ni kama nyingine za Ligi Kuu.

"Hiyo ni mechi kama mechi nyingine ya kawaida, wala hakuna sababu ya kuhofia, sisi Simba si watu wa tambo, lakini ninachosema ni kwamba tunakwenda kushinda mechi hiyo," alisema Try Again.

Bodi ya Ligi tayari imewatangaza waamuzi watakaochezesha mechi hiyo ambao wamechaguliwa na Kamati ya Waamuzi.

Waamuzi hao ni Herry Sasii mwamuzi wa kati kutoka Dar es Salaam, huku waamuzi wasaidizi wakiwa ni Kassim Mpanga wa Dar es Salaam, na Hamdani Said kutoka Mtwara.

Mechi ya mwisho ya Ligi Kuu kati ya timu hizo mbili ilichezwa Septemba 25, mwaka huu Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ilishinda bao 1-0, lililofungwa na Mkongomani Fiston Mayele.

***Imeandaliwa na Adam Fungamwango, Saada Akida na Faustine Feliciane***


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >